

# SISI TUNATAKA KUMWONA YESU



Asante, ndugu. Mwaweza kuketi. Hakika ni majaliwa kuwa hapa katika Grass Valley usiku wa leo, kumwakilisha Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo; kuwaombea watoto wa Mungu walio wagonjwa, mgonjwa wa Daktari; na kuufurahia ushirika huu pamoja, kwa siku hizi tano ambazo tumeahidi.

<sup>2</sup> Ninawaletea salamu kutoka kwa wasafiri hao wengine kutoka sehemu nyingi mbalimbali za ulimwengu ambako nimekuwa. Na nikitumaini...Na maelfu mengi ya watu wanaombea ufanisi wa mkutano huu hapa, siku hizi usiku. Nina hakika, pamoja na maombi ya hao wengine, na sisi wenyewe, kwamba Mungu atakutana nasi na kutubariki.

<sup>3</sup> Na hatuji sasa kuwakilisha kanisa lolote lile, ama hatuji kujiita “waponyaji.” Tunakuja, tukimwakilisha Kristo. Nasi tunakuja, pia, sio kuwaponya wagonjwa, bali kuwaombea wagonjwa, na kufanya tuwezayo kusaidia kufanya maisha yawe rahisi kidogo kwa kila mmoja. Nami nina hakika kwamba mtakuwa baraka kwetu. Nasi tunatumaini kwamba tutakuwa baraka kwenu.

<sup>4</sup> Na sasa nilikuwa tu nikiwazia, tangu tumekuwa huku California katika ziara hii ya mwisho, kwamba imekuwa kwamba watu wanapenda kwenda nyumbani mapema. Sasa, huko nyumbani, na mbalimbali, sehemu nyingi za nchi, unakuta watu ni tofauti. Baadhi yao, wao wanapenda tu kukusikia ukihubiri; sijali kama hata huwaombe wagonjwa, waweke tu yapata saa nne ama tano, ukihubiri, hilo—hilo huwaridhisha tu vema. Lakini huku, hakika inaudhi; wanaonekana tu kama, “Mahubiri mafupi tu, halafu uwaombee wagonjwa, na halafu uturuhusu turudi nyumbani upesi sana maana inanibidi kurudi tena.” Na kila kitu kinaonekana kuharakishwa sana huku. Kwani sote tunaenda wapi? “Haraka, haraka, haraka, haraka, haraka!” Labda, Bwana akipenda, ninataka kuhubiri wakati nikiwa huku, *Kutoa Mvuke*. Nafikiri hilo—hilo ndilo litupasalo kufanya, kidogo tuachilie.

<sup>5</sup> Ndio kwanza nipate ajali, majuma machache yaliyopita. Ninapenda kulenga shabaha, kuwinda. Nilikuwa tu nimepewa bu—bunduki, ambayo ilikuwa imetobolewa tena na Kampuni ya Weatherby hapa chini. Ndipo nikakiinua kitu hicho juu, nipate kurusha risasi, nacho kikalipukia usoni mwangu. Nayo ikaurusha mtutu yapata yadi hamsini, mbele yangu, nao mpini karibu umbali ule ule nyuma yangu, na kuvilipua vichaka na kila

kitu hapo, mahali kitu hicho kilipolipukia. Na ni neema tu ya Mungu haikunilipua jinsi hiyo, maana ilikuwa karibu *hivyo* na macho yangu wakati ilipolipuka, ilivyoning'ia, darubini ikiwa juu, nikipiga risasi.

<sup>6</sup> Ndipo nikapata wazo dogo kutoka kwake. Mnaona, hi—hiyo bunduki kweli haikuwa ni bunduki ya Weatherby. Ilitobolewa tu iwe bunduki ya Weatherby. Ilikuwa ni Winchester ya mtindo wa sabini, kwenu ninyi jamaa mnaowinda. Nayo nilikuwa nimepewa na ndugu mwema wa California jina lake Art Wilson. Alimpa mwanangu, Billy Paul, aina ya Roberts mia mbili na hamsni na saba. Na kwa hiyo wao. . . Billy hutumia mkono wa kushoto, na kamwe asingeweza kuitumia, kwa hiyo akasema, “Baba, nitakupa tu.”

<sup>7</sup> Vema, si—sikuzote nilitaka bunduki ya Weatherby, lakini nilijisikia kana kwamba singemudu kununua moja. Na halafu kama baadhi ya marafiki zangu wangeweza kuninunulia moja, nisingewataka waninunulie, kwa maana ni bunduki ghali. Na kama nilivyosema mara nyingi, “Ninao marafiki wamishenari wasio na viatu miguuni mwao na mimi—mimi siwezi kumwacha mtu alipe gharama hiyo kwa ajili ya bunduki, nipate kuwinda nayo ama kulenga nayo shabaha, wakati nikiwa na marafiki ambao hata hawana viatu.” Kwa hiyo, nisingefanya hivyo kabisa.

<sup>8</sup> Lakini rafiki yangu akasema, “Ninaweza kuichukua hiyo ya mtindo sabini na kufanya bunduki ya Weatherby kutokana nayo. Weatherby hufanya hivyo huko, na kuiwekea dhamana.” Nikasema. . . Kasema haitanigharimu, ila tu yapata “dola kumi, kumi na mbili.”

Kisha nikasema, “Endelea.”

<sup>9</sup> Kwa hiyo akaitoa, akaipeleka kwa kampuni nao wakaitoboa tena. Mara ya kwanza, ililipuka tu. Kwa hiyo haikuwa, hapana budi haikuninii. . . Kitu fulani kilichopata presha mahali fulani.

<sup>10</sup> Sasa funzo langu juu ya jambo hilo ni hili. Mnaona, ilikuwa na presha nyingi kupita kiasi, ikalipuka. Mnaona? Hatutaki presha nyingi kupita kiasi, ita—italipuka.

<sup>11</sup> Na jambo lingine, ningetaka kusema hivi, huenda likaingiza hoja ndogo ya fundisho. Mnaona, kama bunduki hiyo ingalianzia kwenye vifinyangio, ikiwa Weatherby iliyoasiliwa, isingalilipuka. Lakini, mnaona, ilikuwa ni kitu kingine kilibadilishiwa tu njiani, na hiyo ndiyo sababu isingalistahimili presha.

<sup>12</sup> Basi ninaamini katika dini ambayo hatuibandiki viraka. Tunakufa na kuzaliwa mara ya pili, ndipo sisi ni Wakristo wanaoweza kustahimili presha yote ambayo Roho Mtakatifu anataka kuisukuma nje. Kwa hiyo na—nafikiri inatupasa kurudi hapo mwanzo, sio tu kujaribu kufanya kitu fulani kutokana na kitu kisicho. Tuna dini nyingi za kiakili kupita kiasi siku hizi, badala ya ujuzi halisi wa kuzaliwa mara ya pili na Mungu. Na

kwa hiyo mahali fulani barabarani kitu fulani kidogo kitatokea, kitasababisha kuvuja kidogo, na kuilipua presha tena, nawe utajikuta umelipuliwa. Kwa hiyo tunaamini katika kufa hasa kwa nafsi yako na mawazo yako yote na kila kitu kingine, kufa tu kabisa na kumwacha Roho Mtakatifu akufinyange upya. Ninii tu, wewe—wewe ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, hicho ndicho ulicho, kuwa na ujuzi na Mungu kwamba unajua umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Na hicho ndicho tunachoamini.

<sup>13</sup> Tunaamini Biblia, nasi tunaamini kwamba Hicho ni Kitabu cha Mungu. Sisi, sisi tunadumu moja kwa moja na Biblia. Sasa, ninaamini ya kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hajayaandika katika Biblia. Sasa, Yeye ni Mungu, Yeye anaweza kufanya lolote atakalo. Lakini kama ninaweza tu kumwona, maishani mwangu, akitenda yale aliyoahidi, basi ninajua kwamba ni kweli, mnaona, mradi tu liko katika Biblia.

<sup>14</sup> Sasa, katika Agano la Kale, kama vile ndugu wahudumu wajuavyo, kwamba katika u—ukuhani wa Kilawi, walikuwa na njia ya kujua kama nabii alikuwa akisema kweli, ama ndoto ya mwotaji ilikuwa ni ya kweli. Walikuwa na kile kilichoitwa Urimu ya Thumimu. Sasa, hiyo imebishaniwa kwamba ilikuwa ni nini. Lakini hoja iliyo kuu zaidi, iliyo adilifu zaidi niwezayo kuona, na njia inayofaa zaidi, ilikuwa, walichukua naivera aliyovaa Haruni; ambayo iliwakilisha yale makabila kumi na mawili kwa mawe ya kuzaliwa ya yale makabila, nayo ilining'inizwa hekaluni, kwenye nguzo. Halafu basi nabii alipotabiri, ndipo basi wangejua kama ilikuwa ni Kweli, ama sivyo; sasa, kama mkusanyiko huu wa nuru ulimulika mle, alifanya ya Kimbinguni. Mungu ni wa Kimbinguni, kwa sababu Yeye ni Mungu, Roho. Basi kama Nuru hiyo ya Kimbinguni iliwakilishwa mle, kama upinde wa mvua ukimulika kutoka kwenye hii, basi hilo neno, huyo nabii alikuwa sahihi. Hivyo ndivyo alivyotambulishwa, ama mwotaji alikuwa sahihi. Bali iwapo haikumulika kwenye hiyo Urimu ya Thumimu, basi haidhuru ilisikika ya halisi jinsi gani, wao wasingeipokea, kwa sababu haikumulika kwenye Urimu ya Thumimu.

<sup>15</sup> Sasa, ule ukuhani wa Kilawi ulikoma penye mauti ya Bwana Yesu. Sasa tunaishi katika Ukuhani wa Melkisedeki, Kristo. Sasa tungali hatuko bila ya Urimu ya Thumimu. Hii Ndiyo sasa, Biblia. Mnaona, hatuna budi kudumu na Maandiko (sio kuweka fasiri zetu wenyewe Kwake) jinsi tu ilivyoandikwa. Sasa, ninaamini ya kwamba—kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu siku moja kwa Yesu Kristo. Ninaamini hilo. Na—naamini ya kwamba itabidi pawe na kipimo atakachohukumu kwacho, kwa kuwa kuna mengi sana yanayomwakilisha Kristo, na wengi sana.

<sup>16</sup> Sasa, msingi wangu, Mwairishi, kwa hiyo watu wangu kabla yangu walikuwa ni Katoliki. Nilipokuwa mvulana mdogo;

labda mlisoma hadithi ya maisha yangu, wanayo hapa katika vitabu, na kadhalika. Nilienda kwenye kanisa la Kiairishi nami nikasikia yale kasisi aliyosema. Kisha nikaenda kwenye kanisa la Kilutheri, nikasikia yale aliyosema, mchungaji wa Kilutheri. Na kulikuwako na maskini Mbaptisti nyuma mahali fulani katika kizazi chetu, kwa hiyo wao . . . nikaenda kwenye kanisa la Kibaptisti. Nilienda kwenye makanisa mbalimbali. Vema, wao, kila moja, linatofautiana na lingine. Sasa, kila moja lilitaka kusema ya kwamba kanisa hilo lilikuwa sahihi kabisa.

<sup>17</sup> Kwa hiyo, sasa, yote hayawezi kuwa sahihi, hapana budi kuwe na kasoro fulani mahali fulani. Nami ninakuta sasa, kuna yapata madhehebu mbalimbali mia tisa na kitu, kwa hiyo nafikiri hapana shaka kuna kasoro fulani mahali fulani. Maana, kama hili, wote wakiingia kwa kanisa *hili* . . .

<sup>18</sup> Sasa tuliambiwa, kama Wakatoliki, kwamba—kwamba—kwamba “Mungu yuko kanisani Mwake. Na humo ndimo Mungu alimo, katika kanisa Lake.” Kwa hiyo basi kama Mungu yumo katika kanisa Lake, ni lipi baina yao lililo kanisa Lake? Kila moja la hayo husema ndilo “lile kanisa.” Kwa hiyo nilijua jambo moja . . . Basi hilo ni lile tu kasisi alilosema, “Mungu yuko katika kanisa Lake.”

<sup>19</sup> Bali Biblia ilisema, “Mungu yuko katika Neno Lake.” Naye alisema kwamba, “Kila atakayeongeza lolote kwenye Hili, au kuondoa lolote Kwake, huyo ataondolewa katika Kitabu cha Uzima, kwake.” Kwa hiyo ninaamini kwa moyo wangu wote kwamba Neno Hili ni Mungu katika maandishi. Sasa, sababu ya mimi kusema hivyo ni kwa kuwa hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake, yeye si zaidi ya neno lake. Kama huwezi kulichukua neno langu kwa chochote, basi usihusike nami, unaona, kwa sababu huwezi kuniamini. Na hilo ni jambo lile lile, sina budi kuamini kwamba Hili ni Neno la Mungu, nami ninaamini.

<sup>20</sup> Sasa Biblia ilisema, katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu,” basi Huyu alikuwa ni Kristo, naye Kristo ni Neno. Basi kama akiuhukumu ulimwengu kwa Kristo, itabidi iwe ni kwa Neno. Mnaona? Kwa hiyo, hivyo ndivyo tunavyoliamini, na katika mafundisho yetu.

<sup>21</sup> Sasa tutakuwa na mfupi tu, upesi tunavyoweza kutoka . . . Ninii yao ni nini, katika nyakati halisi, ndugu, za kutoka hapa, yapata saa nane ama kitu kama hicho? En-he? Saa nane? Walikuwa wakicheka, kwa hiyo nadhani ni saa tatu ama tatu na nusu, kitu kama hicho, ndio wakati wa kawaida wa kutoka. Hiyo itakuwa ni katika yapata dakika thelathini na tano.

<sup>22</sup> Usiku wa leo, mimi nikiwa ni mgeni miongoni mwenu, hata hivyo sijisikii kwamba mimi ni mgeni. Ninajisikia mimi ni ndugu yenu. Na sasa nawatakeni myafuate yale ninayosema katika

Maandiko. Ndipo Ujumbe labda utakuwa ni tofauti kabisa na yale mmekuwa mkitarajia, bali uchunguzeni na Maandiko. Utafuatilia kabisa mwelekeo ule ule mliosikia. Nitalisoma tu kutoka kwenye Maandiko, halafu nisijaribu kulielezea, niliache tu lijieleze Lenyewe.

<sup>23</sup> Kama vile kuuza bidhaa fulani. Iwapo una bidhaa ya kuuza, kama ina uzuri wowote, itajiuza yenyewe. Haikubidi kufanya matangazo mengi sana kuihusu. Nina mengi sana ya huo upuuzi wa matangazo, ambapo na—naenda kote, naona ninii... kila mtu ni “mtu wa majira haya” na “*huu* ndio ujumbe,” na yote hayo, mpaka ninashangaa kwamba ni nani huyo. Loo, ninaamini Kristo ndiye Mtu wa majira haya, na daima amekuwa. Na majigambo me—mengi sana na upuuzi hayapaswi kuwako.

<sup>24</sup> Nilipata hayo ya kutosha wakati mmoja. Kweni ninyi akina dada... Ni—nina mke wangu, yuko pamoja nasi, na kweli ninampenda pamoja na watoto wangu. Na kwa hiyo daima nataka kumsaidia, nami ni mkono duni sana wa kusaidia. Nami nilikuwa... Ninajua yeye ana mengi sana ya kufanya, na watoto, kuandaa kila kitu, kwenda kulala usiku ninapokuwa nyumbani. Nilifikiri ningemsaidia kuosha vyombo, ila tu ninachukia kufanya hivyo kadiri mnavyochukia. Ndipo nikawazia, “Vema!”

<sup>25</sup> Naye mama alikuwa akinisimamisha juu ya sanduku dogo nipate kuosha vyombo wakati nilipokuwa mvulana mdogo, nami nikawazia, “Kama nikiwahi kuoa, nitaachana na tabia hiyo sasa hivi.”

<sup>26</sup> Lakini hili hapa, ninampenda mke wangu jinsi nilivyompenda mama yangu, ila tu kama mke, na mama yangu. Basi nikawazia, “Vema, nitamsaidia kama nikiweza.”

<sup>27</sup> Ndipo nikaona jambo fulani kwenye kipindi wakati mmoja, ki—kipindi cha televisheni, ambapo nilikuwa nikingojea kwenye—ndege nipate kutoka, nao walikuwa na televisheni imewekwa huko nje na sehemu kubwa sana ya mbele, ikiwa na kioo kikubwa mno, nayo ikasema, “Tumia sabuni fulani hii, hakuna kuosha vyombo, hakuna kusuuza, hakuna kupangusa, hakuna chochote. Vitie tu majini, uvitumbukize ndani, kisha uvitoe, hivyo ndivyo tu inavyokubidi kufanya.”

<sup>28</sup> Nikawaza, “Loo-lo! Mke wangu atanipenda kweli tangu sasa na kuendelea, maana nitamwonyesha jinsi ya kusafisha vyombo.” Kwa hiyo, nikanunua kifurushi chake, kesho yake nilipofika nyumbani. Nikanunua kifurushi kimoja kabla sijafika nyumbani, nikakiweka chini ya koti langu, nikaingia ndani.

<sup>29</sup> Kesho yake asubuhi, nikasema, “Usijali, mpenzi. Nipo papa hapa kukuoshea vyombo. Hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya. Sasa nenda tu upesi huko nje uchukue kifagio na uanze kufagia. Kabla sijaenda ofisini ama kuanza kupiga simu zangu, nitaosha vyombo mara moja.”

<sup>30</sup> Kwa hiyo nikachukua kitu hiki na kusoma juu yake, mwajua, “Tia vijiko viwili vya mezani vilivyojaa.” Nami nikawaza, “Jamani, nitaifanyia kazi nzuri sana,” nikamwaga yapata—yapata nusu ya kifurushi hicho mle ndani, nikakoroga namna *hiyo*; nikaokota vyombo vyote na kuvitumbukiza ndani namna hiyo, mapovu yakatokea juu *hivyo*. Nikawaza, “Jamani, dakika chache tu sasa, na yote yanipasayo kufanya ni kuvitoa na kuviweka mezani tena.” Watoto walikuwa wamekula mayai kwa ajili ya kiamshakinywa; nikavitoa, kulikuwa na mayai mengi kadiri yalivyowahi kuwapo.

<sup>31</sup> Kwa hiyo nikasema, “Nikiona kitu chochote kimetangazwa sana, nitakiacha tu tangu hapo na kuendelea, sitajisumbua, kwa sababu ninajua hakifanyi hayo.”

<sup>32</sup> Na kwa hiyo wakati mwingine nafikiri kwamba kama tukizungumza tu habari za Yesu na kuwaacha watu waone kwamba Yeye ni Nani, na kile—kile alichu, basi ninaamini kwamba hiyo itaninii. . . Yeye, Yeye atafanya yaliyosalia. Yeye, Yeye atajileta Mwenyewe, maana, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, kwa vyovyote vile.” Mnaona, hilo ndilo Yesu alilosema. “Wala hakuna mtu awezaye kuja asipoitwa na Baba Yangu.” Kwa hiyo jambo pekee tufanyalo ni kupanda tu Mbegu, na kuiachilia.

Sasa, ninatumaini kwamba mtashika simu na kuwaita watu.

<sup>33</sup> Nalo jambo muhimu hapa sio kuwaombea wagonjwa sasa, hilo ni moja ya mambo ya pembeni, lakini jambo muhimu ni kumfanya kila mwenye dhambi tuwezaye kumjua Bwana Yesu kama Mwokozi wake. Hilo ndilo jambo muhimu. La pili, ni kumfanya kila mtu ambaye amempokea Kristo kama Mwokozi wao, na hajajazwa na Roho Mtakatifu, wapate kujazwa na Roho Mtakatifu. Na hilo—hilo ndilo lenu la pili. Kisha jambo la tatu, ni kuwaombea wagonjwa wote tuwezao kuwaombea. Na, kupitia hilo, tunatumaini ya kwamba Mungu atatupatia wakati mkuu sana katika mkutano huu. Nami nafikiri ni kila jioni kisha Jumapili alasiri, nafikiri, ni—ni kweli.

<sup>34</sup> Ninataka kuwashukuru ndugu zangu hapa, wahudumu, kwa kunialika hapa. Nami namshukuru Mungu kwa uongozi wa kuja huku. Sasa, meneja hapa, Bw. Borders, tulikuwa na kitabu kilichojaa mialiko ya kote duniani, bali kwa namna fulani kitu Fulani kikasema nami kuhusu Grass Valley.

<sup>35</sup> Na mara moja, rafiki yangu, ile familia ya Arganbright huku chini katika Los Angeles, alinipigia simu na kusema, “Endapo hujafanya ratiba yako kabisa ya kupitia, laiti ungalisimama Grass Valley.”

<sup>36</sup> Nikampigia meneja simu, nikamleta kwenye simu, nikasema, “Umepitia kule hata hivyo?”

“La.”

Nikasema, “Pitia mle.” Basi sisi hapa.

<sup>37</sup> Sasa yale Bwana atakayofanya, sijui mimi. Huenda kuna mtu mmoja hapa Yeye anamtafuta, anayemjia. Natumaini Yeye amekuja kuiokoa jamii nzima.

<sup>38</sup> Sasa, juu ya hili, na tuinamishe vichwa vyetu na kunena na Mwandishi wake kabla hatujalisoma Neno Lake.

<sup>39</sup> Baba yetu wa Mbinguni, kweli ni majaliwa tuliyo nayo, kusimama Uweponi Mwako, katika majira haya ya kumalizia kwa historia ya ulimwengu huu, na kukuita Wewe “Baba,” na kujua ya kwamba tu—tunakukaribia Wewe kwa Njia itoshelezayo kwa yote, pamoja na hakikisho lililobarikiwa kwamba Yesu, Mwana Wako, alisema, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya, mtapewa.” Ndipo tunajua, Baba, kama tukiomba katika Jina la Bwana Yesu, kwamba ombi letu litakidhiwa. Sasa tusingetaka kuomba lolote kinyume na mapenzi Yako. Ila tunaamini, baada ya Wewe kutuongoza hapa, ya kwamba ni mapenzi Yako kuwaokoa watu, na kuwaponya watu, na kuwajaza watu na Roho Mtakatifu, na kujitwalia Mwenyewe utukufu. Nasi tupo hapa kufanya kila kitu ambacho Wewe unatuongoza kufanya. Kwa hiyo ninaomba, Baba, kwamba utalifunua Neno Lako kwetu, na mapenzi Yako, pamoja na Neno Lako, tupate kujua yaliyo mapenzi Yako kuhusu Neno Lako. Tubariki pamoja sasa. Zisamehe dhambi zetu.

<sup>40</sup> Basi usiku wa leo, tunapoketi kwenye jengo hili, tunaomba ya kwamba Wewe utalibariki jengo hili. Mungu, labda ni uwanja wa maonyesho, bali sasa unawekwa wakfu kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu, upate kuwa nyumba ya kanisa ambapo heshima na upendo na uchaji unapewa Mwenyezi. Tujalie, Bwana, kwamba kila mtu anayepitia kwenye milango hii katika siku hizi tano ama sita zijazo, ataingia chini ya sadikisho hivi kwamba hata hawataweza kuondoka kwenye jengo hili pasipo kuutoa moyo wao kwa Kristo.

<sup>41</sup> Tunaomba, Baba, kwamba kila mgonjwa anayeingia katika jengo hili, na wale wanaoingia wakiwa na wengine moyoni mwao, wakiomba, ya kwamba Bwana Yesu mbarikiwa atakuwako kuwaponya wagonjwa. Ujaze moyo wa kila mtu na Roho Mtakatifu.

<sup>42</sup> Pia, Mungu, wavute ndani kutoka kwenye ulimwengu huu mlevi, wenye kichaa cha kuipenda dhambi, unaopenda anasa, kabla haijachelewa kupita kiasi, kabla milima haijafanywa tambarare, kabla ile ghadhabu kuu ya Mungu kumwagwa juu ya kizazi kisichoamini. Mungu, lilete karibu sana nasi juma hili tupate kuliona, nayo mioyo yetu itajazwa kabisa, hata kila mtu aliye humu ndani atakuwa mhudumu mtaani na katika ujirani, kuwaleta wengine kwa Kristo.

<sup>43</sup> Hatujui kama kamwe tutaumaliza uamsho hapa, ama la, mpaka Wewe utakapokuja. Ila tunajua jambo hili moja, kwamba

siku moja Wewe utakuja, nasi hatujui hiyo itakuwa ni saa gani. Lakini jalia tuishi kila saa ili kwamba, kama ilikuwa ni saa hiyo, tungekuwa tayari kwenda na kusimama Uweponi Mwako, kusikia ikisemwa, “Ilikuwa vema, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu; ingia katika furaha za Bwana, ulizoandaliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Tunajiweka wakfu, pamoja na jengo hili, na Neno Lako, kwa heshima na utukufu wa Mungu, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

<sup>44</sup> Bwana awabariki. Sasa tungependa kusoma Maandiko fulani hapa, yanayopatikana katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu, mlango wa 12 na kifungu cha 20.

<sup>45</sup> Na wazo le—letu katika hili, ninii. . . wazo la uamsho wetu ni kwamba, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Sasa, hiyo ni Waebrania 13:8, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Sasa Yohana Mtakatifu 12:20.

*. . . palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea wakaenda kwenye. . . sikukuu:*

*Basi hao wakamwendea. . . Filipino, mtu wa Bethesda, Bethsaida ya Galilaya, wakamwambia, wakisema, Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

<sup>46</sup> Sasa, nataka kutoa sasa, kwa dakika chache zijazo, mazungumzo mafupi tu ya kawaida, katika kufanya na kuweka msingi. Tutaanzia, tuseme, juu ya uponyaji wa Kiungu. Na daima, Yesu, ninaamini, katika huduma Yake, yapata asilimia themanini yake, ilikuwa juu ya uponyaji wa Kiungu.

<sup>47</sup> Na kama vile maskini rafiki yangu mzee, Ndugu Bosworth, ambaye wengi wenu Wakristo mlimfahamu, yeye alizoea kusema, “Sikuzote, kuvua samaki, huwaonyeshi ndoana, unawaonyesha chambo. Ndipo samaki anarukia chambo, na anapata ndoana.”

<sup>48</sup> Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyojaribu kuwashika Wakristo kwa ajili ya Kristo, ni kwa miujiza ya uponyaji wa Kiungu, kuonyesha uwepo Wake. Halafu basi, katika hilo, wanajua ya kwamba mwanadamu hawezi kufanya mambo hayo, kwa hiyo linaishika nafsi ya mwaminio, naye analikubali juu ya misingi hiyo. Kwa hiyo sasa, kwanza, ninataka kutoa mazungumzo ya kusema kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

Nao hawa Wayunani walisema, “Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.”

<sup>49</sup> Sasa, hao Wayunani wangeonyesha mawazo yetu vizuri hapa usiku wa leo. Siamini kunaye mtu hapa ila yule ambaye angetaka kumwona Yesu Kristo. Kutaka tu kujua ni wangapi hapa ndani ambao wamewahi kusikia habari Zake, wangetaka kumwona, ninakutaka tu uinue mkono wako. Angalieni tu, ni asilimia mia moja. Hakuna mtu anayeweza kusikia habari Zake. . . Jina hilo tu la kupendeza sana hutufanya kutamani kumwona!

<sup>50</sup> Kuna jambo fulani kumhusu Kristo ambalo haliko na watu wengine. Yeye alikuwa ni tofauti. Alikuwa ni Mwana wa Mungu. Na kuna—kuna jambo fulani tofauti sana kumhusu Yeye ambalo watu wengine hawaonekani kuwa nalo kama Yeye alivyokuwa nalo. Nasi tunaye Roho, tunafahamu, bali tunaye kwa kipimo. Yeye anaye pasipo kipimo. Yeye alikuwa ni Imanueli, Mungu akiishi katika mwili wa Kristo Yesu, Mungu akidhihirishwa katika mwili. Kristo alikuwa sura ya Mungu iliyodhihirishwa, akimdhihirisha Mungu kwa watu. Alichokuwa Mungu, walikiona katika Kristo, Mwana Wake. Yeye alikuwa yule Mtiwa mafuta. Neno *Kristo* linamaanisha “Mtiwa mafuta.”

<sup>51</sup> Na sasa kama Wayunani hao, wakimtafuta Yeye... Sasa, sasa hebu tutafakari juu ya kila Neno. Wayunani hao, wakimtafuta Yesu, walimjia mmoja wa wanafunzi Wake, ambaye alikuwa ni Filipo, wa Bethsaida. Na yeye—yeye alikuwa akimtafuta Yesu, kwa hiyo akamjia mwanafunzi, naye huyo mwanafunzi akampeleka kwa Yesu. Kama hiyo ilikuwa ndiyo njia ya kumwona Yesu, kwa hao Wayunani, nasi tunataka kumwona Yesu yuyo huyo, nayo Biblia inasema “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” basi mbona hatuwezi kumwona? Sasa ninyi...

<sup>52</sup> Maandiko hayawezi kusema uongo. Hayo ni Kweli. Ninaamini hilo. Na kama Maandiko haya yalikuwa ni ya uongo, basi ngingekuwa nikifanya jambo lingine usiku wa leo mbali na kusimama hapa nikiliwakilisha Hili. Lakini ninaamini ya kwamba Hayo ni ya kweli, kweli kabisa. Hayahitaji tafsiri yoyote. Yako tu jinsi yanavyopaswa kuwa, yameandikwa tu mumu humu ndani, maana Mungu amehakikisha ya kwamba yamekaa jinsi hiyo. Sasa angalieni.

<sup>53</sup> Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Mungu hana kikomo, yuna nguvu zote, yuko kila mahali, anajua yote? Hakika. Sasa, Yeye ni Mungu, kwa hiyo uamuzi Wake wa kwanza juu ya chochote hauna budi kudumu vile vile, kwa sababu maamuzi Yake yangekuwa ni makamilifu, kwa sababu Yeye hawezi kufanya lolote ila ukamilifu. Hivyo ndivyo tu alivyo, ni ukamilifu. Kamwe hawezi kubadilika. Sasa hapa ndipo matumaini yetu yamejengwa juu ya Neno. Kama Mungu aliwahi kuitwa jukwaani, kufanya uamuzi kuhusu jambo lolote lile, uamuzi Wake wa kwanza hauna budi kudumu vile vile milele. Kamwe hauwezi kubadilika. Kabla tu hatujalifikia wazo hilo, wazieni jambo hili.

<sup>54</sup> Wakati Mungu, katika bustani ya Edeni, hapo alipoitwa kwa ajili ya wokovu wa Adamu na Hawa, Yeye alikuwa na tiba moja, hiyo ilikuwa ni damu. Na kamwe hajaibadilisha. Milele, ni—ni damu! Kamwe hawezi kuibadilisha.

<sup>55</sup> Wakati Mungu alipoitwa, kumponya mgonjwa, Yeye alimponya kwa imani yake. Na Yeye hawezi kamwe kuibadilisha.

Mnaona? Na kama alimponya mtu mmoja, kwa sababu ya imani yake katika Mungu kufanya hivyo, basi itambidi kumponya huyo mwingine, la sivyo alitenda vibaya alipomponya wa kwanza, na alitenda vibaya alipomwoko wa kwanza. Mnaona? Kwa hiyo huwezi...

<sup>56</sup> Sisi hubadilika. Sisi ni—sisi ni kile mnachoita “wenye kikomo.” Na Yeye ni Asiye na Kikomo. Kwa hiyo hawezi kubadilika, kwa sababu Yeye ni mkamilifu. Sisi hufanya uamuzi, kisha tunaona, “Vema, *huo* ulikuwa mbaya. Nitaufanya *hivi*, uwe bora zaidi.” Bali si Yeye. Wake wa kwanza ni mkamilifu. Hivyo ndivyo unavyopaswa kubaki daima. Kwa hiyo Yeye hawezi kujifunza zaidi wala kuwa mwerevu zaidi, kama tunavyofikiri sisi hufanya, bali Yeye ni mkamilifu tangu mwanzo.

<sup>57</sup> Sasa tunasikia mengi sana kuhusu Yesu siku hizi, na kila uendako. Sasa, mimi ni mmishenari, mnafahamu; hii ni mara yangu ya saba kuizunguka. Sasa, hii katika huduma ya umishenari, tunawaona watu wakiabudu sanamu na kadhalika, na mamilioni yao. Lakini hapa Marekani tunaona makanisa kwenye kila pembe, kila moja likiwakilisha Mungu kwa njia fulani, nao wanapata maoni mengi sana mbalimbali kulihusu. Wengine wanajaribu kumpata Mungu kwa njia moja, na wengine nyingine. Hakika ipo njia sahihi mahali fulani. Hapana budi pawe na njia sahihi mahali fulani.

<sup>58</sup> Kwa sababu, kama vile Daudi alivyosema, “Kilindi kinapoita Kilindi, hapana budi pawepo, kwanza, kitu fulani cha kuitikia wito huo, la sivyo huo wito usingekuwapo.” Kwa maneno mengine, hapana budi pawe na Muumba kabla hapajakuwapo na uumbaji. Mnaona? Hapana budi pawe na kitu Fulani kilichoweka uumbaji ndani yako, hapo kabla; Muumba kuweka uumbaji, halafu basi hapana budi pawe na kitu cha kuitikia hilo. Kabla hapajakuwapo na pe—pe—pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi pawe na maji kwanza apate kuogelea, la sivyo asingekuwa na pezi. Kabla hapajakuwapo na mti wa kukua duniani, ilibidi pawe na ardhi, kwanza. Na mradi kuna njaa moyoni mwa mwanadamu, kwa ajili ya Mungu, hapana budi kuwe na Mungu mahali fulani kuitikia wito huo.

<sup>59</sup> Na wengi wapo hapa usiku wa leo wakitafuta uponyaji wa Kiungu. Mbona mnautafuta? Kwa sababu kitu fulani ndani yako kinakwambia, “Kuna Chemichemi mahali fulani.” Unaona? Na mradi kuna kitu fulani ndani yako, kikikwambia, “Kuna Chemichemi mahali fulani,” hapana budi pawe na Chemichemi hiyo, la sivyo kamwe kusingekuwako na shauku hiyo ndani yako. Mnaona, Muumba, kuumba kiumbe.

<sup>60</sup> Sasa tunaona watu katika siku hii, wakitamani, wakivuta, wakikimbia hapa na pale, wakitafuta, wakinyakua, wakibadilisha makanisa, wakibadilisha makaratasi na madhehebu mbalimbali, na kadhalika. Kuna shida gani?

Wana njaa ya kitu Fulani, lakini hawaonekani kupata kile wanachoonea njaa. Hapana budi kuwapo na Kitu hicho mahali fulani.

<sup>61</sup> Sasa, wengine siku hizi wanamtafuta Mungu kupitia kanuni zao za imani. Watu wengine wanafikiri, kupitia kwa kanuni zao za imani, watapitia tu “Katika kanuni fulani ya imani, hiyo humpata Mungu.” Wengine wanafikiri, “Kujiunga na madhehebu fulani, kunampata Mungu.”

<sup>62</sup> Vema, Yesu alikuta jambo lilo hilo alipokuja duniani. Yeye aliwakuta Mafarisayo, Masadukayo, na wowote zaidi, yale mashirika mbalimbali, ama madhehebu na kanuni za imani za siku hizo. Aliwaambia nini? “Kwa mapokeo yenu mmezitangua Amri za Mungu.” Mnaona?

<sup>63</sup> Nafikiri kwamba kumtafuta Mungu kupitia kwa kanuni za imani ama kupitia kwa madhehebu, jambo pekee lifanyalo, hulifanya kuwa la kisiri sana, kisha unapata kwamba linarudi moja kwa moja na kulikana Neno, linarudi moja kwa moja na kuzitangua Amri za Mungu. Kwa mfano, unajaribu kumpata Mungu kwa kukariri Kanuni ya Imani ya Mitume. Kisha unarudi kupata Marko 16 kufanywa halisi kwako, “ishara hizi zitafuatana na hao waaminio”; mbona, watakwambia upesi sana, “Vema, hizo siku za miujiza zimepita!” Basi inafanya nini? Inazichukua Amri za Mungu na kuzitangua; mnaona, hazina nguvu, Amri za Mungu.

<sup>64</sup> Amri Yake, ambayo ni, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Sasa, Injili haikuja kwa Neno tu, bali kwa madhihirisho ya Neno, madhihirisho ya Roho Mtakatifu akilifanya Neno liishi. Mnaona, ni Roho akilichukua Neno.

<sup>65</sup> Neno lilikuwa ni wazo. Nalo wazo ni...Neno ni wazo lililotamkwa. Mnaona? Sasa, yalikuwa ni mawazo ya Mungu, yale Yeye aliyokuwa akitaka kufanya, kisha akayaelezea kwenye Neno.

<sup>66</sup> Na sasa wakati Roho Mtakatifu anapolishika Neno, Yeye hulitimiza na kulidhihirisha, na kulifanya halisi, kila Neno la Mungu. Hakuna Andiko ila lile lililotolewa kwa uvuvio! Na kila Neno la Mungu ni kamilifu na ni sahihi, nalo litatimizwa. Kila Neno halina budi kutimizwa. “Mbingu na nchi zitapita,” kasema Yesu, “bali Maneno Yangu hayatahindwa.” Kila Neno Lake halina budi kutimizwa.

<sup>67</sup> Sasa, ndipo wakati Mungu anapofanya hivyo, nasi tunaona kanuni yetu ya imani basi, kama tukisema kanuni fulani za imani ama vitu fulani ambavyo sisi ni wafuasi wake...Na mimi sina lolote dhidi ya hilo. Hilo ni sawa.

<sup>68</sup> Ni kama tu kula tikitimaji, kama vile yule mtu mweusi alivyosema hapo alipokula kipande chake. Alisema, “Unaonaje juu yake, Mose?”

<sup>69</sup> Akasema, “Ni tamu, bali hakika kuna nyingine zaidi.” Kwa hiyo, haikutosha kuridhisha.

<sup>70</sup> Kanuni ya imani ni sawa, bali kamwe hairidhishi mpaka unapofikia kwenye Neno. “Na mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Hilo ndilo mtu atakaloishi kwalo. Neno la Mungu ni Mkate wa kiroho wa kila siku wa mwanadamu, ni Neno la Mungu lililodhihirishwa.

<sup>71</sup> Na wakati Mungu alipowapa Israeli ile nchi ya ahadi, wakati walipokuwa wangali Misri, iliwabidi kupigania kila inchi ya nchi hiyo. Mungu alimwambia Yoshua, katika Yoshua 1, “Popote nyayo za miguu yako zitakapokanyaga, hiyo nimekupa kama urithi.” Kwa hiyo, *alama za miguu* zinamaanisha “umiliki.” Watu wengine wanaweza tu kufikia, angalau kufikia u—ukingoni tu mwa nchi hiyo. Wengine wanaweza kuchukua Upanga wenye mikono miwili na kuwafyeka Wafilisti na Waamori mpaka wakiteke kitu hicho chote. Hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya. Kila ahadi ni kwa ajili yetu. Tuna...Alama za miguu ni umilikaji. Kwea moja kwa moja na uiteke! Mungu alitupa sisi. Ni ahadi na ni Kweli, na ni kwa ajili yetu.

<sup>72</sup> Sasa, kisha katika kanuni hizi za imani, wanakuja huku tena, kama nisemavyo, na kufanya, kwa mapokeo yao, kuzitangua Amri za Mungu. Hufanya, huziondolea mbali, wanazielezea vinginevyo.

<sup>73</sup> Lakini hakika kuna njia ya kujua yaliyo Kweli, kwa sababu Maandiko hapa yanasema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Sasa, huwezi kulichukua Andiko hilo na kuliondoa kwenye Biblia. Huna budi kuliacha katika Biblia, maana ni la humo ndani. Na kama Hilo likisema, “Ni yeye yule,” halimaanishi Yeye ni yule yule nusu, linamaanisha kwamba “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

<sup>74</sup> Sasa, basi, tunataka kuona. Ningependa kumwona akiya humu jengoni usiku wa leo. Ningependa kumwona. Nanyi je? Tulisema muda mfupi uliopita, tunataka. Sisi tunataka kumwona Yeye. Vema, basi, kama Yeye alituhidi hilo, kwa nini tusimwone? Hiyo ni i-...Sasa, kama tutayafungua tu macho yetu na nia zetu kwa muda mfupi tu, ninaamini kwamba tutaewa, na Yeye ataingia na kujitambulisa Mwenyewe pamoja nasi. Sasa, na kisha tungeondoka usiku wa leo, tukisema, “Tunataka kumwona Yesu.”

<sup>75</sup> Walimpata wapi Yesu katika Agano la Kale; moja kwa moja katika Agano Jipya, ninamaanisha? Moja kwa moja na Neno, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. Sasa, Yeye hakuwa Neno katika njia waliyokuwa wameliweka pamoja, bali alikuwa ni Neno katika njia ambayo Mungu aliliweka pamoja, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno lililo hai.

<sup>76</sup> Sasa, wakati alipokutana na Shetani, Yeye alikutana naye kwenye Neno. Yeye—Yeye—Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili; bali wakati alipokutana na Shetani kamwe hakutumia Nguvu Zake za—za Uungu Wake, kile Yeye alichokuwa. Alisema, “Imeandikwa, ‘Mtu hataishi kwa mkate pekee.’ Imeandikwa, ‘Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye pekee.’” Alipokutana na Shetani, alikutana naye kwa Neno, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. Sasa, Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Sasa, Musa alinena habari Zake katika Neno, sasa, katika Kumbukumbu la Torati, mlango wa 18, kifungu cha 15.

<sup>77</sup> Musa aliandika vile Vitabu Vitano vya Agano la Kale, Kutoka na Mwanzo; Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Kumbukumbu la Torati, Hesabu. Aliandika Vitabu Vitano vya—vya Agano la Kale. Mle ndani, kwa uvuvio kutoka kwa Mungu, aliandika na kusema *yaliyokuwako*, kisha akaandika na kusema *yatahayokuwako*. Nayo yale aliyosema *yangekuwako*, yalitimia; kwa hiyo tunajua kwamba yale aliyosema *yaliyokuwako*, ni kweli. Kwa kuwa mwanadamu anaweza kutazama *huku* na kuona yale yatahayotukia, na kama yakitukia, basi yale aliyosema *huko* nyuma hakika yalikuwa yamevuviwa pia.

<sup>78</sup> Sasa, Wayahudi wote walifundishwa kuwaamini manabii wao. Wangali wanawaamini. Kama Paulo alivyosema, “Wayahudi hutafuta ishara, nao Wayunani hekima, na kadhalika. Sisi tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa.”

<sup>79</sup> Sasa, Biblia ilikuwa imewafundisha hao Wayahudi, “Akiweko mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho, ama nabii, mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake. Na—na katika unabii na maono, ndoto, na kadhalika, na yale asemayo yakitimia, basi msikieni.” Sasa, hiyo ni wazi tu. “Lakini yasipotimia kama alivyosema, basi msimsikie.” Maana, Mungu hawezi kusema uongo, Yeye ni Mungu. Lakini kama mtu akisema jambo fulani, nalo linatimia, halafu mliangalie ndani yake, likitimia, likitimia, likitimia, basi mnajua kwamba hiyo haiwezi kuwa ni mtu huyo. Hiyo haina budi kuwa ni Mungu. Kwa hiyo Mungu aliwaambia manabii... ama, aliwaambia Wayahudi kumsikiliza mtu huyo, kwa sababu alikuwa ni nabii aliyetumwa kutoka kwa Mungu.

<sup>80</sup> Sasa, Musa alikuwa ni nabii yule mkuu. Hatuna wakati wa kuingilia hilo, maisha yake, kuonyesha jinsi alivyomfananisha Kristo. Lakini alikuwa nabii mkuu. Naye alisema ya kwamba, “Bwana Mungu wako atamwinua Nabii kama nilivyo mimi. Itakuwa kwamba yeye asiyemsikia Huyu atakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa watu.” Sasa, sasa kama Musa alinena, na manabii wengine... Naye Musa, kumbukeni, aliandika Mwanzo, pia. Kutoka katika bustani ya Edeni, “Uzao wa mwanamke utakiponda kichwa cha nyoka,” na ahadi zote huko nyuma za Masihi ajaye, Musa aliziandika. Halafu hao manabii wengine,

wakuu, kama Isaya, Yereima, na kadhalika, wote walinena kuhusu Masihi ajaye. Manabii, ambao, maneno yao yalitimia. Sasa, wao walinena na kusema Yeye angekuwa ni Nabii hapo atakapokuja. “Atakuwa ni Nabii kama nilivyo mimi,” Musa alisema. Hivyo ndivyo Yeye angekuwa.

<sup>81</sup> Sasa, kama tungetaka kumwona Yesu leo hii, nayo Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” basi kuna njia moja tu ya kulifanya. Sio . . .

<sup>82</sup> Tuweke tu kando kanuni zetu za imani kwa ninii chache, kwa saa moja sasa, ama nusu saa. Tuweke kando kanuni zetu za imani, tuweke kando maoni yetu ya kimadhehebu, na kadhalika, na hebu turudi nyuma tuone kile Yeye alichokuwa. Sasa hilo lingekuwa . . . Hilo lingekuwa la maana, sivyo? Hilo lingekuwa ni zuri. Twende tutafute kujua kile Yeye alichokuwa, na ndipo tutajua kile alichokuwa ikiwa tunaweza kujua kile alichokuwa. Lakini njia pekee utakayoninii . . . Kama Yeye alikuwa ni kanuni ya imani huko nyuma, basi kanuni hiyo ya imani ni sahihi. Kama Yeye alikuwa ni dhehebu huko nyuma, basi hiyo ni sahihi. Tafuta kujua lilikuwa ni dhehebu gani ama ilikuwa ni kanuni gani ya imani.

<sup>83</sup> Lakini tunaona, huko nyuma Yeye alikuwa ni Neno, kwa hiyo Yeye angali ni Neno. Sasa nilisoma kutoka Yohana Mtakatifu. Sasa kama tukirudi hapa nyuma kwenye mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu, na tutachukua tu baadhi ya Yale, kile Yeye alichokuwa, kutoka kwenye mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu. Sasa tunaona ya kwamba, “Hapo mwanzo alikuwako Neno,” kama nilivyonukuu tayari, “naye Neno alikuwa ni Mungu; huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa ni Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu.” Sasa tunaona kile Yeye alichokuwa. Sasa tuna “Neno likiwa ni Mungu,” na “Mungu akifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu,” katika siku hizo. Sasa Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana . . .” Hiyo ilikuwa ni Agano Jipya.

<sup>84</sup> Katika Agano la Kale, Kristo, vile vile. Kristo, yeye yule katika Agano Jipya. Naye Kristo, yeye yule, hata milele. Basi kama tunaweza kuona “kile Yeye alichokuwa,” basi “kile Yeye alichokuwa,” na “kile Yeye atakachokuwa,” basi tumelipata. Hiyo ni kweli?

<sup>85</sup> Musa alisema, sasa, “Yeye atakuwa kama mimi, Nabii mithili yangu.” Ndipo Yeye alipokuja, kile Kristo *alichokuwa*, ilibidi awe kile Yeye . . . Basi ilibidi awe kile Yeye alichokuwa kabla ya hapo. Kwa hiyo sasa hebu tuanze kutoka papo hapo, ndipo tutaona kile Yeye atakachokuwa milele. Hiyo ndiyo njia pekee ya kulifanya.

<sup>86</sup> Yeye yule jana, sasa alikuwa ndiye huyu hapa, tunaona yule mwandishi wa Waebrania, ni Paulo, akisema, “Yesu Kristo yeye yule jana,” akizungumza na Waebrania. Nasi sote tunajua ya

kwamba Yehova wa Agano la Kale, alikuwa ni Yesu wa lile Jipya, na ndiye Roho Mtakatifu wa siku hizi. Ni Mungu yeye yule akijidhihirisha tu katika ofisi tatu mbalimbali. Na, kwa hiyo, Mungu yeye yule! Na yote aliyokuwa Mungu, aliyamwaga katika Kristo, yote aliyokuwa Kristo, aliyamwaga katika Kanisa. Kwa hiyo, mnaona, mnaweza kuona upesi kile Yeye alichio, “Yeye yule jana, leo, na hata milele.”

<sup>87</sup> Sasa, bali inatubidi kupata tabia Yake, kile alichokuwa. Sasa sote tunajua, na wasomaji wote wa Biblia watakubali, kwamba Nguzo ile ya Moto iliyowafuata Israeli nyikani, ama wao waliifuata ile Nguzo ya Moto, hasa, kwamba huyo alikuwa ni Malaika wa Agano aliyezungumza na Musa katika kichaka kilichowaka moto, Nguzo ile ile ya Moto. Ninzi, mnakubaliana na hilo? Sote tunakubaliana. Vema, Malaika wa Agano ni Nani? Kristo. “Musa aliiacha Misri, akihesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa ni hazina kuu kuliko zile za Misri.” Mnaona?

<sup>88</sup> Na sasa wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, ile Nguzo ya Moto ilifanyika mwili, ikakaa miongoni mwetu. Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Nilitoka kwa Mungu, na naenda kwa Mungu.” Sasa kumbukeni, “jana, leo,” mnaona. Yeye alitoka kwa Mungu, kutoka kwenye ile Nguzo ya Moto, anarudi kwa Mungu.

<sup>89</sup> Sasa, baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Sauli wa Tarso, akienda zake Dameski, kuwakamata wapentekoste, akienda zake kule, kulifanyika nini? Nguzo ya Moto, Nuru ilimwangusha chini. Hakuna mtu mwingine aliyeiona. Yeye aliiona. Iliyapofusha macho yake kwa muda fulani. Ilikuwa ni halisi sana kwake; wakati hao wengine waliosimama pale, wasingeweza kuona kitu; lakini ilikuwa angavu sana kwake, iliyapofusha macho yake. Ndipo Yeye akasema, “Sauli, Sauli, mbona unanitesa Mimi?”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?” Sasa sikilizeni!

<sup>90</sup> “Mimi ni Yesu. Na ni vigumu kwako kupiga teke michokoo.” Mnakumbuka hilo. Vema, Yeye huyu hapa, Nguzo ile ile ya Moto *iliyokuwako*.

<sup>91</sup> Basi iwapo Yeye ni yule yule “jana,”; basi katika siku za Paulo, “leo”; Yeye atakuwa yeye yule “milele”! Kwa hiyo ile Nguzo Kuu ya Moto, Mungu, yule Malaika wa agano, ni yeye yule leo kama alivyokuwa wakati alipowaongoza Israeli. Tazama!

<sup>92</sup> Sasa tutaanza huduma Yake, katika Yohana Mtakatifu 1. Tunajua... Tutaruka wito na kuzaliwa Kwake, na Yohana Mbatizaji, na kuuendea ubatizo Wake, kisha akaingia nyikani, akajaribiwa na ibilisi, akarudi baada ya siku arobaini mchana na usiku za kufunga nyikani. Akarudi na kuanza huduma Yake. Sasa hebu—hebu tuifuatilie huduma Yake hapa. Mara, watu wakaanza kupona walipoombewa, na Yeye.

<sup>93</sup> Basi tunaona kwamba kulikuwako na mtu jina lake Simoni, naye alikuja kwa Yesu kwa kualikwa na kaka yake, Andrea. Basi alipoenda Mbele za Yesu. . . Sasa kumbukeni, huyu hapa mtu muhimu anakuja. Sasa tunafahamu, kulingana na Matendo mlango wa 4, kwamba yeye alikuwa mtu asiye na elimu wala maarifa. Tunafundishwa ya kwamba asingeweza hata kuandika jina lake mwenyewe. Sasa, yeye hakuwa mwanachuoni. Hakuwa askofu. Hakuwa ku—kuhani. Alikuwa ni mvuvi.

<sup>94</sup> Mungu daima huchukua kitu ambacho ni duni, na kufanya kitu fulani kutoka kwake. Yeye hujidhihirisha Mwenyewe kupitia kitu bure, kusudi mtu yeyote aweze kuona kwamba ni Mungu. Mnaona, Yeye huchukua kitu bure.

<sup>95</sup> Basi Yeye alimchukua huyu mtu asiye na elimu. Sasa atamfanyaje mtu huyu kujua ya kwamba Yeye yuko? Maana, mambo mengi bandia yalikuwa yamefanyika. Na tumekuwa nayo kote katika nyakati.

<sup>96</sup> Na kila wakati unapoichukua dola bandia, na kuiangalia hiyo dola bandia, kumbuka tu ya kwamba dola hiyo bandia imefanyizwa kwa dola iliyo halisi. Kwa maana kama hakukuwako na dola halisi, basi dola hiyo bandia ingekuwa ndiyo na—nakala halisi. Mnaona? Kwa hiyo mradi tu unamwona mtu akiigiza ama kutekeleza sehemu ya mnaofiki, kumbuka tu kuna Mkristo halisi mahali fulani. Unaona? Ukiona mtu akitambulisha namna fulani ya mfumo wa kidini wa mungu wa u—uongo, ama namna fulani ya mhemuko wa ki—kiakili, kidini, kumbuka tu, nyuma kule, mahali fulani, yupo Mungu halisi, wa kweli. Angalia. Loo, ninalipenda tu! Tazameni.

<sup>97</sup> Sasa mara, mara tu Simoni. . . Hebu tuchukue mchezo mdogo wa kuigiza wa kishamba ya Simoni, kwa dakika moja, akiwa ni mzee. Baba yake alikuwa ni mzee, pia. Na labda siku moja, kama nilivyosoma hadithi yake ndogo; baba yake alikuwa ni mvuvi, naye alikuwa akivuta ndani. Walikuwa wana haja na samaki, sana. Kwa hiyo wao, siku hiyo wakawavua wengi sana. Sikuzote waliomba kabla hawajaenda kuvua samaki. Na kwa hiyo yeye alikuwa na madeni ya kulipa, ndipo akashika lu—lundo kubwa la samaki. Ndipo akaketi chini kando ya mtumbwi na kumkumbatia Simoni, na kusema, "Simoni!" Jina lake lilikuwa ni Yona, mwajua. Ndipo akasema, "Simoni, mvulana wangu, nimefikiria kwamba siku moja nitamwona Masihi. Hayo yamekuwa ndiyo matumaini ya watu wetu tangu tulipotoka Misri, ama tangu tulipojua kulikuwako na Masihi aliyeahidiwa. Miaka elfu nne imepita, mwanangu. Watu wengi mashuhuri, manabii, wamekufa, wakimtazamia. Nilifikiria Yeye angekuja katika kizazi changu. Lakini ninazeeka sasa, labda sitamwona. Lakini, Simoni, ninataka ukumbuke, wewe na Andrea, ya kwamba Yeye labda atakuja katika kizazi chenu, kwa kuwa mimi ni mzee sasa na niko tayari kwenda kuwa pamoja na watu wangu. Nami nimejaribu kuwalea ninzi wavulana vizuri,

nimejaribu kuwalea katika Neno. Sasa sikilizeni. Sasa, Simoni na Andrea, kabla Masihi huyo kweli hajainuka, kutakuwako na mambo mengi sana yatakayoendelea chini ya jina la ‘Masihi,’ kwa sababu huyo atakuwa ni adui. Bali usisahau, Simoni, wewe pamoja na Andrea sikuzote dumuni pamoja na Neno. Msiliache Neno. Kumbukeni, Masihi atakuwa nabii kama Musa, kwa kuwa hiyo ni kweli kabisa. Haijalishi, huenda akawa jitu kubwa la kidini, naye huenda akaweza kuyaelezea maneno, huenda akaweza kufanya kitu chochote kama hicho; bali Biblia ilisema, ‘Yeye atakuwa ni Nabii kama Musa.’ Amina. Sasa hivyo ndivyo utakavyomjua.”

<sup>98</sup> Basi siku hiyo wakati Simoni alipoenda huko, pamoja na Andrea, Mbele Zake, naye Yesu amesimama pale, Ambaye Andrea alikuwa amemwambia, “Tumempata Masihi.”

<sup>99</sup> Basi ningewazia Petro alifikiria hivi, ama Simoni, kama alivyokuwa wakati huo, “Sasa labda umechanganyikiwa kabisa, Andrea. Nitaambatana nawe, nami nitajua.”

<sup>100</sup> Kwa hiyo wakati alipoenda mbele za Yesu, Yesu alisema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.”

<sup>101</sup> Hilo lilitosha. Hilo lilikuwa ndilo. Alimwamini na kumkubali Yeye, hivi kwamba alikuwa na funguo za Ufalme baadaye. Hakuchukua masomo yoyote au chochote kile, alikuwa na funguo za Ufalme. Kwa sababu, kwa ufunuo wa Mungu yeye alijua kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi, kwa sababu alikuwa ni Masihi wa Kimaandiko. Yeye alikuwa ni nabii, nao hawakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne, tangu Malaki. Walikuwa na manabii wa uongo. Lakini, nabii wa kweli aliyesema Kweli! Na huyu hapa Mtu alikuwa amesimama hapa Ambaye, mara alipomwona, hakujua tu yeye alikuwa ni nani, bali alijua baba yake mzee mtauwa aliyekuwa amemfundisha alikuwa ni nani. Hilo lilitosha! “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu.” Mnaona?

<sup>102</sup> “Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona.” Hilo lilitosha kumwonyesha. Sasa hilo ndilo Yesu alilofanya jana, kujithibitisha Mwenyewe, kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

<sup>103</sup> Kulikuwa na mmoja aliyesimama pale. Tutaharakisha. Kulikuwa na mmoja aliyesimama pale, jina lake Filipo. Mbona, lilimchangamsha! Huyo ndiye tunayesoma habari zake hapa. Lilimchangamsha sana! Sasa, huenda Filipo alisema, “Aisee, hilo, hilo latosha! Sasa nina hakika!”

<sup>104</sup> Moja kwa moja akakizunguka kile kilima, maili kumi na tano. Alikuwa na rafiki ambaye alikuwa ameenda shuleni pamoja naye, mtu mwema, mtu wa Maandiko, mtu mwadilifu, mtu aliyejua Maandiko, na kumpenda Mungu. Nami ninaweza kumwona akibisha mlango, na—na kusema, “Yuko wapi Nathanaeli?” [Ndugu Branham anagongagonga mimbara—Mh.]

105 Mkewe akasema, “Yuko huko nje u—uani huko nje. Anaomba.”

106 Akaenda kumtafuta, naye alikuwa chini ya mti. Basi alipompata, alisema, “Njoo, mwone Mtu tuliyempata; Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu.”

107 Na sasa ninaweza kumwazia Filipino, ama, Nathanaeli akisema, “Sasa, Filipino, laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?”

Akasema, “Njoo uone.”

108 Sasa, hilo ni tamshi zuri kwa mtu yeyote. Usikae nyumbani na kukosoa. Usiamke na kuondoka. Kaa na ungoje, uone kama ni Kweli, ama siyo. Mnaona? “Njoo, ujionee mwenyewe.”

109 Vema, akapiga kona; hebu tuwazie mazungumzo yao. Ninaweza kumsikia Filipino a—akimwambia Nathanaeli, “Nathanaeli, Maandiko yanasema Masihi atakuwa nini?”

“Loo, Yeye atakuwa—Yeye atakuwa Nabii kama Musa.”

110 “Hakika. Hiyo ni kweli. Vema, huyu Yesu wa Nazareti ninayekwambia habari Zake, unamkumbuka yule mzee mvua samaki uliyenunua samaki kwake, naye asingeweza kutia sahihi ya jina lake?”

111 “Naam. Loo, hakika, yule mwana wa Yona. Ninamfahamu vizuri. Jina Lake ni Simoni.”

112 “Mara alipoenda Mbele za Mtu huyu, Yeye alimwambia yeye ni nani, na kuhusu baba yake. Haingenishangaza kwamba Yeye asingekwambia wewe ni nani,” akasema.

“Vema,” akasema, “sasa, hebu kidogo. Itanibidi kuona hilo.”

113 Vema, hatimaye, wakafika mkutanoni. Mara alipoenda Mbele za Yesu, Yesu alisema, “Tazama, Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

114 Sasa huenda ulisema, “Vema, hakika, Yeye anajua ni Mwisraeli, jinsi alivyovalia.” Wamashariki wote huvalia vile vile, wote wana rangi nyeusi, na walikuwa na ndevu, na kilemba, na—na majoho, na kadhalika, vile vile tu. Basi Yeye angejua yeye alikuwa ni mtu mwaminifu, asiye na hila?

115 Yeye alisema, Yeye alimwambia, “Tazama, Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

116 Nalo likamshangaza mtu huyo wa Kimaandiko. Akasema, “Rabi,” ambalo linamaanisha *mwalimu*, “ulinijua lini Wewe? Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Ulinijua lini Wewe?”

117 Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.” Haya basi. Jambo ndilo hilo. “Nilikuona,” maili kumi na tano kuuzunguka mlima, siku moja kabla. “Nilikuona ulipokuwa chini ya mti.” Sasa, unajua yale aliyofanya? Alimkimbilia, akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu! Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli!” Hiyo ndiyo ile saa.

Kwa nini? Yeye ni wa Kimaandiko, Yule ambaye nabii alisema angekuja. “Wewe ni Mwana wa Mungu! Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli!” Haileti tofauti yoyote yale hao wengine waliyosema.

118 Sasa, kulikuwako na wale waliokuwa wamesimama pale, loo, Mafarisayo na Masadukayo, na maaskofu, na chochote zaidi, viongozi, viongozi wakuu wa kidini, makuhani wakuu, na makuhani, na chochote zaidi, wamesimama karibu pale, nao wakaliangalia Hilo. Walijua iliwabidi kutoa jibu kwa kusanyiko lao. Iliwabidi kuwatolea swa- . . . iliwabidi kujibu swali lao. Kwa hiyo unajua walichosema? Walisema, “Mtu huyu ni Beelzebuli.” Mnaona? Kwa maneno mengine, “Yeye ni mpiga ramli, ibilisi.”

119 Ndipo Yesu akawageukia, akasema, “Nitawasamehe.” Mnaona, walimwita Roho wa Mungu, aliyekuwa akifanya hivyo, roho mchafu. Kasema, “Nitawasamehe kwa kufanya hivyo. Lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja kufanya jambo lile lile, na neno moja dhidi Yake halitasamehewa katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.” Neno moja dhidi Yake. Sasa, hilo lilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine. Waangalieni.

120 Sasa, Biblia ilisema ya kwamba “Neno la Mungu,” Waebrania 4, “ni kali kuliko upanga ukatao kuwili. Neno, ambalo lilikuwa ni Kristo, kali kuliko upanga ukatao kuwili, ukikata hata kwenye mafuta ya mfupa, na Huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Neno! Wakati Neno Lenyewe linaposonga mbele, hivyo ndivyo lilivyo. Hilo ndilo tangazo, hilo ndilo thibitisho la Neno. Basi hapo Neno lilikuwa limesimama pale, lililofanyika mwili miongoni mwao, likifanya vile hasa Hilo lilisema litafanya, nao hawakulitambua Hilo.

121 Sasa, kumbukeni, kuna jamii tatu tu za watu duniani, hizo ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Tunajua hilo, kama tunaamini Biblia. Wote walianza kutokana na hao watoto watatu, watoto wa Nuhu; Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

122 Mliona Petro akiwa na zile funguo za Ufalme? Wa kwanza aliowafungulia, walikuwa ni Wayahudi, huko Pentekoste. Hiyo ni kweli? Na wakati Filipo aliposhuka akaenda kuwahubiria Wasamaria, walikuwa wamebatizwa katika Jina la Bwana Yesu, bali hawakuwa wamempokea Roho Mtakatifu bado; ndipo wakatuma mtu na kumfanya Petro ashuke aende naye akawawekea mikono, wakampokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli? Matendo 10:49, “Petro alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia hao waliolisikia Neno.” Mnaona? Sasa waangalieni hao watu watatu: Wayahudi, Wamataifa, na Wasamaria.

123 Sasa hapa Wayahudi na Wasamaria walikuwa wakimtaamia Masihi. Sasa Yesu alikuwa akienda Zake Yeriko, kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko, bali alikuwa na haja ya kupitia Samaria.

<sup>124</sup> Sasa kumbukeni Yohana Mtakatifu 5:19, Yesu alisema, baada ya kupita kwenye birika la Bethesda, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda.” Mlilipata? Yesu alisema, “Mwana hawezi kutenda Neno Mwenyewe,” hiyo ni *Yeye*, “bali yale Mimi,” sio *kumsikia* Baba, bali, “kumwona Baba analitenda.” Sasa, Andiko hilo ni la kweli, la sivyo hayo mengine huenda yakawa ni ya uongo. Yeye alisema, “Kabla sijafanya lolote, mimi huona kwa ono yale Baba anayonionyesha Mimi kufanya, ndipo ninaenda na kuyafanya.” Mnaona? Wote walikuwa wamemzunguka. “Lakini ninyi, hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba.” Hiyo ni kweli.

<sup>125</sup> Kwa hiyo alikuwa na haja ya kupitia Samaria, ndipo Yeye akakwea maeneo ya Samaria. Nayo ilikuwa yapata saa sita. Ndipo akawatuma wanafunzi Wake mle ndani, alipofika kwenye mji wa Sikari, na Yeye akawatuma wanafunzi Wake mle kununua vyakula, mlo. Basi wakati walipokuwa wameondoka, mwanamke wa Sikari akatokea.

<sup>126</sup> Sasa, yeye alikuwa ni mwanamke ambaye tungemwita “mwanamke mwenye sifa mbaya,” labda msichana mrembo, aliyepitia njia mbaya, naye alikuwa akiishi maisha mabaya. Basi akatoka aende kuchota maji. Maana, hawezi kutoka... Nimekuwa humo nchini mimi mwenyewe, nazo mila zao zingali ni zile zile. Mwanamke wa aina hiyo hashirikiani na wanawake waadilifu; kwa hiyo hawezi, hawezi kuja kisimani wakati ule ule wakiwa mle, au kitu fulani. Na kwa hiyo—kwa hiyo alikuja kisimani baada ya hao wanawake wengine kuchota maji yao, akaja kuchota maji.

<sup>127</sup> Basi alipokuja, yeye alisimama, naye alikuwa akishusha winchi, nayo ina viopoo viwili, na kuiweka tu juu ya mpini wa chungu, namna *hii*. Si ndoo; ni kitu kama chungu, kitu kama hicho, kilichofinyangwa kwa udongo, nao wanakishusha kisimani, na kukipandisha juu kwa winchi. Basi akaanza kuishusha hiyo ndoo, ndipo akamsikia Mtu akisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.” Ndipo akatazama huko. Kidogo ilikuwa ni maskini mandhari kama hii hapa, ambapo kisima cha mji cha umma kiko huko nje, nje ya Sikari. Ndipo basi akaangalia huko, na huyo hapo Myahudi mwenye umri wa makamu ameketi. Sasa, Yeye kweli alikuwa tu na yapata miaka thelathini na miwili.

<sup>128</sup> Lakini alikuwa ndio kwanza apitie, katika Yohana Mtakatifu 6, ambapo walimwambia alionekana kana kwamba alikuwa na hamsini. Lakini, hakika, kazi Yake ilikuwa imesababisha hilo, labda. Kasema, “Wewe ni Mtu asiyeziidi umri wa miaka hamsini, na unasema Wewe ‘ulimwona Ibrahimu’? Tunajua ya kwamba Wewe una kichaa sasa.”

<sup>129</sup> Akasema, “Kabla ya Ibrahimu kuwako, MIMI NIKO.” Hiyo

ni kweli. Hawakulielewa Hilo, ingawa walikuwa wa kidini na wenye akili walivyoweza kuwa. Lakini akili sio kumjua Mungu; huna budi kusahau hayo yote, upate kumjua Mungu. La.

<sup>130</sup> Nao hao hapo. Kwa hiyo mwanamke huyu akasema... Sasa, yeye alikuwa kile tunachoita siku hizi, “kahaba,” naye huyo hapo. Akasema, “Bwana, si kawaida kwenu Wayahudi kuniomba mimi, mwanamke wa Samaria, chochote, kwa sababu hatuna uhusiano.” Kwa maneno mengine, “Kuna ubaguzi.”

<sup>131</sup> Yeye akasema, “Mwanamke, kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukizungumza naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Ninge kupi maji usije hapa kuyachota.” Yeye alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake.

<sup>132</sup> Sasa kumbukeni, Yeye alikuwa na haja kwenda hadi Samaria. Baba alisema tu, “Kwea uende Samaria.” Hakufanya chochote mpaka Baba alipomwonyesha.

<sup>133</sup> Sasa Yeye huyu hapa Samaria. Sasa Yeye hajui yale hasa yatakatokua, lakini huyu hapa mwanamke, kwa hiyo akawazia Yeye angeendeleza tu mazungumzo naye. Kwa hiyo akasema, akaanza kuzungumza juu ya maji ya kunywa. Mwanamke akaanza kuzungumza juu ya kuabudu kwenye mlima *huu* ama mlima *ule*, ama kadhalika. Mara moja akashika tatizo lake lilikuwa nini. Ni wangapi wanaojua lilikuwa ni nini? Hakika, yeye alikuwa na waume watano, sita, hasa. Kwa hiyo akasema... Akasema, “Nenda, kamwite mume wako, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

<sup>134</sup> Akasema, “Hiyo ni kweli. Umesema vema, kwa maana umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Hapo umesema kweli.”

<sup>135</sup> Tazameni! Sasa sina budi kushindilia hili kabisa, maana sina budi—sina budi kuondoka. Angalieni tofauti kati ya mwanamke huyo, katika hali hiyo aliyokuwamo, na hao wahudumu waliostaarabika sana.

Mwanamke huyu alisema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.”

<sup>136</sup> Hao makuhani na wenye elimu walisema, “Wewe ni Beelizebuli, ibilisi, mpiga ramli.”

<sup>137</sup> Mwanamke huyu alisema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatuambia mambo haya.”

<sup>138</sup> Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, haina budi kuwa ni ile ile!

<sup>139</sup> Akasema, “Tunamjua Masihi, aitwaye Kristo, Yule aliyetiwa mafuta; ajapo, Yeye atatuambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe?”

140 Akasema, “Mimi Ndiye ninayesema nawe.” Hilo lilitosha. Akalionia!

141 Angalia tofauti. Angalieni hapo Nuru hiyo ilipomulika juu ya hiyo mbegu ya kidini na kanuni za imani, na kimadhehebu, haikuwa na matokeo hata kidogo. Lakini wakati wa kwanza Nuru hiyo ilipomulika juu ya maskini ile mbegu iliyochaguliwa tangu zamani pale, ilimulika upesi, yeye akaitambua Hiyo. Akasema, “Bwana, hapana shaka Wewe ni Nabii! Tunajua Masihi yuaja, na Yeye atafanya mambo hayo.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

142 Naye huyo akaondoka, akaingia mjini, kasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Amina.

143 Haya basi! Yeye alikuwa nini jana? Hivyo ndivyo Yeye alivyo leo, na atakuwa milele. Mnaona? Alikuwa.

144 Daudi alitiwa mafuta kwa Roho wa Mungu. Manabii walitiwa mafuta kwa Roho wa Mungu.

145 Huyu alikuwa ni Kristo katika Yusufu, ambaye alimfanya aonyeshe picha ya Kristo, kikamilifu. Aliuzwa kwa vipande thelathini vya fedha, akapendwa na baba yake, akachukiwa na nduguze, katika nyumba hii ya gereza. Kama vile Kristo alivyokuwa msalabani, mmoja aliokolewa; nao mchinjaji na mtunzaji vileo, basi mmoja aliokolewa na mwingine akapotea, jambo lile lile. Akaketi mkono wa kuume wa Farao; na kila wakati alipojitokeza, baragumu ililia, “Kila mtu pigeni goti. Yusufu yuaja.” Hakuna mtu angaliweza kumfikia Farao, ila kwa Yusufu tu. Huyu alikuwa ni Kristo ndani ya Yusufu!

146 Huyu alikuwa ni Kristo ndani ya Daudi, kama mfalme aliyekataliwa, ndipo akapanda juu kwenye kilele cha Mlima wa Mizeitumi wakati alipokuwa ameng’olewa mamlakani huko chini na watu wake mwenyewe, na mfalme aliyekataliwa, akapanda juu ya kilima na kuililia Yerusalemu, na kulia, kwa sababu yeye alikuwa mfalme aliyekataliwa. Roho yuyo huyo ndani ya Kristo, alilia juu ya Yerusalemu, na kusema, “Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi ningewakusanya kama kuku afanyavyo.”

147 Ilikuwa ni Kristo katika watu hao, wapakwa mafuta, wakija, mpaka huyu Mpakwa mafuta mkamilifu akaja. Dhabihu ya dhambi haikuwa imetolewa. Asingeweza kuja katika mwili wote jinsi hiyo, kwa sababu ilikuwa tu chini. . . Wao walikuwa wametiwa mafuta. Lakini sasa Roho Mtakatifu amekuja, ambaye ni Kristo katika umbo la Roho. Sasa angalieni.

148 Sasa, kwa nini Yeye hakufanya ishara hizo kwa ajili ya Mataifa? Kamwe haikufanywa na Yeye. Kwa nini? Mataifa hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote. Walikuwa ni makafiri, sisi tulikuwa, watu wetu, Warumi na kadhalika, huko nyuma

wakiwa na rungu mgongoni mwao, wakiabudu sanamu. Hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote. Naye Masihi huwajia wale tu wanaomtazamia. Hiyo ndiyo njia pekee. “Kwao wanaomtazamia, Yeye ataonekana mara ya pili.” Wale tu wanaomtazamia! Sio tu wale—wale wanaofaa; bali wale wanaomtazamia Yeye kweli. Pia angalieni, Yeye kamwe hakuja kwa Mataifa. Mwijiza huo kamwe haukufanywa mbele za Mmataifa.

<sup>149</sup> Naye Mungu asiyebadilika! Sasa tumekuwa na miaka elfu mbili ya masomo na kila namna ya mambo, na sasa imefikia wakati wa jioni, na sasa Mataifa yanamtazamia Masihi ajaye. Sasa, kama Yeye ni yeye yule! Alionekana yeye yule wakati huo, kwa hayo makabila mawili, hana budi kuonekana jinsi iyo hiyo pale. Na aliahidi, hata hivyo! Andiko moja zaidi, kisha nitafunga.

<sup>150</sup> Sikuzote kumbukeni, wekeni matabaka matatu ya watu niani mwenu. Daima yapo, hayo ni: waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Wako katika kila kundi. Mnaona?

<sup>151</sup> Basi Ibrahimu alipewa ahadi, pamoja na uzao wa Ibrahimu baada yake. Sasa angalieni uzao wa Ibrahimu, katika mfano wa Lutu, alishuka akaingia Sodoma, anasa za ulimwengu; hilo ni kanisa la kawaida, la kimadhehebu, la shirika. Lakini Kanisa la kiroho, ambalo lilikuwa ni Ibrahimu ambaye Mungu alimtembelea mwenyewe, wale walioitwa watoke, kamwe yeye hakingia Sodoma, alikuwa nje ya Sodoma; hilo ni Kanisa, lililoitwa litoke. Sasa, wakati wa mwisho ukatimia, wakati alipokuwa akitaka kuziangamiza nchi kwa moto.

<sup>152</sup> Hivyo ndivyo Yeye anajitayarisha kufanya tena. Hiyo ni kweli? Sasa tazama. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Kumbukeni, hayo yalikuwa ni mataifa ya Kimataifa. Mnaona? Ule mwisho, kama ilivyokuwa katika Sodoma. Sasa hawa hapa Mataifa wakija. Wakati wa Kiyahudi uliangamizwa kwa maji. Wakati huu, Mataifa wanaangamizwa kwa—kwa moto. Angalieni, “kama ilivyokuwa katika Sodoma,” hebu tuangalie tu.

<sup>153</sup> Huyu hapo Ibrahimu, lile Kanisa teule, lililoitwa litoke Sodoma; la kiroho, Mungu akiwatokea kambini mwao wakati wote, ishara na maajabu, pamoja na ahadi. Limeketi hapa juu vilimani, nchi kame, si tajiri wala si kama hayo mengine; bali maskini, limekaa kule juu; maskini kundi dogo, lililodharauliwa, lililodhihakiwa. Hayo mengine yalikuwa yameenda na kutajirika, nao ni watawala wa mji, kama vile watoto wa Kaini walivyofanya sikuzote, watu wakuu, wanasayansi, madaktari, na kadhalika. Hao hapo, kama vile tu wamekuwa sikuzote. Mungu habadiliki. Nao hao hapo wameketi pale.

154 Sasa, huko chini Sodoma kulikuwako na kanisa vuguvugu, Lutu na kundi lake. Ibrahimu na kundi lake walikuwa ni Kanisa teule. Angalieni. Ndipo basi Wasodoma, wasioamini.

155 Basi kukaja Wajumbe watatu kutoka Mbinguni, wamevalia kama wanadamu. Naye Ibrahimu alikuwa ameketi mlangoni pa hema lake asubuhi moja, naye akaangalia, ndipo Wanaume watatu wakakaribia. Sasa, walikuwa na mavumbi nguoni mwao, kana kwamba walikuwa wakisafiri. Naye Ibrahimu, kulikuwako na Kitu fulani kidogo ndani yake, yeye alijua ya kwamba hao walikuwa ni wageni. Walionekana kama mtu fulani ambaye anapaswa kumtambua, kwa hiyo akatoka mbio.

156 Kuna jambo fulani kuhusu Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili, unapokutana na mmoja! Nilikuwa nikipitia kwenye mkahawa leo hii, mtu fulani akasema, “Mungu akubariki.” Nikageuka. Nikasema, “Aa-loo, kuna shida.” Maskini mama mmoja akanipa mkono. Sasa, jambo fulani kuhusu Mkristo aliyezaliwa mara ya pili!

157 Basi Malaika hawa wakaenda kule wakaanza kuzungumza na Ibrahimu. Sasa kumbukeni, wawili wao walishuka wakaenda Sodoma, wakawaite watoke, waone kama wangeweza kupata watu kumi wenye haki. Hiyo ni kweli? Wawili wao wakaondoka. Mmoja wao akabaki nyuma na kuzungumza na Ibrahimu. Hiyo ni kweli? Sasa tazama.

158 Huko chini, hakukuwako na miujiza yoyote, waliwapiga tu kwa upofu walipokuja kuingia ndani. Nako kuhubiriwa kwa Injili kweli humpiga asiyeamini kwa upofu. Hivyo ndivyo Biblia isemavyo. Basi kumbukeni, Billy Graham mamboleo na wenyewe akili huko chini wakihubiri, “Tokeni! Tokeni! Tokeni!” Mnaona?

159 Lakini kumbukeni, yule Mmoja aliyebaki nyuma na Ibrahimu, alifanya jambo lingine na Kanisa teule, alikuwa ameketi huku mgongo wake umeelekezwa kwenye hema. Sasa kumbukeni, yeye alikuwa “Abramu” hadi siku moja ama mbili tu kabla ya hapo, naye Sara alikuwa “S-a-r-a-i.” Lakini sasa yeye ni *S-a-r-a*, naye *I-b-r-a-h-i-m-u*; “baba wa mataifa,” na “binti mfalme.” Mnaona? Sasa huyu Mgeni alijua, wakati alipoketi chini, huku mgongo wake umeelekezwa kwenye hema? Ndipo Yeye akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Alijua alikuwa ameo? Alijua jina lake lilikuwa Sara?

Ndipo Ibrahimu akasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

160 Sasa tazama. “Mimi,” kiwakilishi nafsi, “Nitakuzuru.” Alikuwa amefanya nini? Akaketi hapo akala ndama ambaye Ibrahimu alichinja, akala mkate ambao Sara alioka, na kunywa maziwa kutoka kwa ng’ombe.

161 Mtu fulani aliniambia sio muda mrefu uliopita, kasema, “Kwani huyo alikuwa ni nani, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Alikuwa ni Mungu.”

<sup>162</sup> Ibrahimu anapaswa kujua, alizungumza na Yeye. Mwulize mhudumu yeyote. Alimwita, “Elohimu,” a—aishiye peke Yake; herufi kubwa B-w-a-n-a, “Bwana,” aishiye peke Yake.

<sup>163</sup> Sasa angalieni, hamtalikosa. “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

Kasema, “Yuko hemani, nyuma Yako.”

<sup>164</sup> Kasema, “Nitakuzuru kulingana na wakati wa uhai.” Kile alichomwahidi miaka ishirini na mitano hapo kabla! Ibrahimu alikuwa na mia moja, naye Sara tisini. “Nitakutembelea kulingana na uhai.”

<sup>165</sup> Sasa kumbukeni, Sara, mwanamke mkongwe, ilikuwa imekoma kuwa kwake kama mke. Hakuna mwanamke mwenye umri wa miaka tisini... Labda miaka ishirini ama thelathini, labda, tangu alipokuwa mke kwa Ibrahimu. Walikuwa ni wakongwe. Naye akacheka moyoni mwake; mwajua, kile tunachokiita, “kucheka kifichifichi.” Kasema, “Mimi, mwanamke mkongwe kama nilivyo; na bwana wangu, Ibrahimu, huko nje, mkongwe, pia; nami nipate raha kama bibi-arusi tena, na Ibrahimu?” Ndipo akacheka juu ya jambo hili.

<sup>166</sup> Naye Malaika, huku mgongo wake umegeuzwa kuelekea kwenye hema, kasema, “Mbona Sara akacheka, akisema ya kwamba, ‘Mambo haya hayawezekani?’” Hiyo ilikuwa ni telepathia ya namna gani?

<sup>167</sup> Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Hapo, kanisa la kawaida lina wajumbe wao. Naye Mjumbe wa Roho Mtakatifu yuko pamoja na Kanisa teule, akifanya jambo lile lile, ambalo linamfanya Yeye, Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mjumbe wa wakati huu ni nani? Hakuna mtu! Roho Mtakatifu ndiye Mjumbe wa wakati huu. Ni kitu gani? Mungu, akiishi katika mwili wa binadamu. Utukufu! Ninajisikia kubarikiwa. Amina. Mungu, katika mwili wa kibinadamu, akiishi miongoni mweni!

<sup>168</sup> Yesu alisema, “Lo, bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena.” Huyu ni asiyeamini. “Hata hivyo ninyi mtaniona,” Kanisa, “kwa kuwa Mimi,” kiwakilishi nafsi tena, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa wakati, mwisho wa ulimwengu.” Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele! Mungu wetu hajafa! Yeye yu hai milele! Yeye anaishi katika wakati wa mwisho, wakati jua likitua.

<sup>169</sup> Jua sikuzote huchomoza Mashariki na kutua Magharibi. Ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Tunajua hilo. Ustaarabu wa kale sana tulio nao ni Uchina. Ndipo wakati Mwana (M-w-a-n-a) alipoangaza kwa mara Yake ya kwanza, ilikuwa ni juu ya watu wa Mashariki. Sasa ustaarabu umesafiri hata tumefikia...

Moja kwa moja ng'ambo ni Pwani ya Magharibi! Tukienda mbali zaidi, tutatokea Mashariki tena. Kituo kinachofuata ni Japani, Uchina. Tutakuwa Mashariki tena, kama tukienda mbele zaidi. Ustaarabu umesafiri pamoja—pamoja na jua.

<sup>170</sup> Sasa nabii alisema, “Kutakuwako na siku ambayo haiwezi kuitwa mchana wala usiku, siku yenye utusitusi, yenye ukungu.” Watu wamejua vya kutosha kumhusu Mungu kujiunga na kanisa, kuweka jina lao katika kitabu, kutembea katika Nuru ile waliyokuwa nayo. Katika siku yenye ukungu, kuna kiasi fulani cha jua, la sivyo usingeweza kutembea hata kidogo. Lakini yeye alisema, “Katika wakati wa jioni, itakuwa Nuru.” Ni kitu gani? Jua lile lile linalochomoza Mashariki, hutua Magharibi. Naye Mwana wa Mungu yule yule aliyedhihirishwa na kutokea Mashariki, anaonekana Magharibi sasa katika wakati wa jioni, Nuru ya jioni kwa Kanisa lililoitwa litoke na kujazwa na Roho Mtakatifu.

<sup>171</sup> Kristo, kwa Damu na Nguvu za mishipa Yake Mwenyewe, aliwasafisha watu wachafu, naye anaishi miongoni mwao katika mfano wa Roho Mtakatifu. Amina. Picha Yake, ni wangapi wamewahi kuiona ile picha? Iko moja kwa moja huko nyuma sasa. Unaweza kwenda ukaiangalie. George J. Lacy, mkubwa wa FBI katika alama za kidole, imepigwa. Naye Malaika yule yule aliyewaongoza Israeli, yupo hapa sasa akitenda na kufanya jambo lile lile alilolifanya hapo alipokuwa katika Utu wa Yesu Kristo. Kristo, ule mwili, amepaa juu hata kwenye mkono wa kuume wa Baba; lakini Roho Mtakatifu amerudi, Uhai uliokuwa ndani ya Kristo, uko ndani ya Kanisa. Sasa Kristo hakuninii . . . Vema, kama . . .

<sup>172</sup> Wakati Yesu aliposema, katika Yohana 15, “Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi.” Sasa, Mzabibu hauzai tunda; ni tawi. Mnajua hilo, ninyi watu hapa, ninyi wakulima wa mzabibu, na kadhalika. Sasa, kama tawi hilo la kwanza lililotoka kwenye Mzabibu, lilizaa Kitabu cha Matendo nyuma yake, lile Kanisa la kwanza; kama Mzabibu huo ukiwahi kutoa lingine, tawi lingine, litaandika Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake. Kwa kuwa, Uhai wenyewe ulioko katika Mzabibu huzaa ndani ya tawi. Hakika. Tuna matawi mengi sana yaliyopandikizwa hapa ndani.

<sup>173</sup> Niliona mti hivi majuzi huko Phoenix, Arizona, uliokuwa na matunda tisa mbalimbali juu yake, matunda jamii ya chungwa. Nami nikamwambia mtu fulani, nikasema, “Ndugu Sharrit.” Nikasema, “Ndugu Sharrit, huo ni, huo ni kitu gani? Ndimu, chenza, kangaju, na—na balungi, na kila kitu.” Nikasema, “Sasa wakati hayo, hayo yote yamechumwa,” nikasema, “mwaka ujao basi utazaa, utazaa machungwa, maana ni mchungwa.”

<sup>174</sup> Kasema, “Loo, la. Utazaa balungi, ndimu, na chochote hilo tawi lilicho.”

175 “Mbona,” nikasema, “hiyo ni ajabu. Unataka kusema uliupotosha mchungwa huo ukawa miti ya aina hiyo?”

176 Akasema, “La. Mchungwa ungali ni mchungwa. Kama ukiwahi kuzaa tawi lingine, litazaa chungwa. Lakini lile limepandikizwa ndani yake namna hiyo, linazaa kwa jinsi yake, kwa sababu ni tunda jamii ya chungwa.”

Nikasema, “Haya basi!”

177 Dhehebu linaweza tu kuzaa tunda la kimadhehebu. Lakini kama Mzabibu huo asilia kamwe ukizaa lingine, itakuwa ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele! “Nitarudisha,” asema Bwana. Amina. (Ni wakati wa kwenda nyumbani.)

178 Ati nini? “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Ungemtafuta mtu wa aina gani? Mtu wa aina ile ile huyo alivyokuwa. Sasa, hushuki kwenda mtaani hapa na kumtafuta m—mtu aliyevalia namna fulani ya joho, na makovu ya misumari kichwani mwake, ama chochote kile. Mnafiki yeyote anaweza kufanya hilo. Na hiyo ni kweli. Mtu yeyote anaweza kuiga hilo. Lakini ingekuwa ni ule Uzima uliokuwamo ndani ya Kristo, utakuwa ndani ya Kanisa Lake. Jambo ndilo hilo, ule Uzima!

179 Kama uliuchukua uhai kutoka kwenye bo—boga, na kuuweka katika mbalungi, utazaa maboga, kama ungeweza kuishi namna hiyo. Hakika, uhai ulio ndani yake.

180 Na hapo ndipo Uhai ulipo sasa. Uhai wa Kristo ndani ya Kanisa, utamzaa Kristo tena. Hivyo ndivyo wanavyomwona Kristo. Ninii... Katika Yohana 14:12, yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, sio anayejifanya kuamini; bali yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Nyingi kuliko hizi atazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu.” Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

181 Wakristo. Nimekuwa mmishenari, nimeona mamia ya miungu mbalimbali, naam, maelfu yao, kila namna, Makalasinga, Majaini, Budha, wote wa namna zingine waliowekwa pamoja, mnaona. Nilikaribishwa hapa si muda mrefu uliopita, huko India, ambako nilikuwa na umati ulio mkubwa kuliko wote, laki tano katika kusanyiko moja. Na huko nilikaribishwa katika hekalu la Wajaini. Na humo ndani mlikuwamo na dini kumi na saba mbalimbali, miungu kumi na saba mbalimbali, na kila mmoja wao akiupinga Ukristo. Lakini, loo, jamani, mngepaswa kumwona Yeye akiya jukwaani. Kila mmoja wa waanzilishi wao amekufa na hayuko. Wetu alifufuka tena, Naye yu hai milele, akiishi Kanisani Mwake, yeye yule jana, leo, na hata milele.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

182 Bwana Yesu, tuna furaha sana kuzungumza habari Zako. Wewe unapendeza sana na unastahili sana yote tuwezayo kusema. Lakini, Baba, Neno moja tu kutoka Kwako lingefanya

mengi kuliko yote ningaliweza kusema, au mhudumu mwingine yeyote. Neno moja tu kutoka Kwako lingelitatua. Hivi hutafanya jambo hilo usiku wa leo, Baba, tunapokungojea Wewe, sasa, kwa muda mfupi tu, naomba. Tutangojea, hatutakungojea dakika moja, Bwana, tutangojea mpaka Wewe utakapokuwa tayari. Tunataka kusikia kutoka Kwako. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, usiku wa leo, kwa kuwa nimeliweka kusanyiko tena, muda mrefu. Lakini wao wanapendeza sana, Bwana. Nami ninajua jua la jioni limetua. Tunaishi tu katika vivuli sasa. Pia, Mungu, huenda kukawa na mtu asiyekujua Wewe. Ninaomba ya kwamba Wewe utakuja kwetu usiku wa leo, Bwana, katika umbo la Roho Mtakatifu, na uwajalie watu wakuone Wewe, wamwone Yesu yeye yule waliyemwona katika siku zilizopita.

<sup>183</sup> Haikuwa ni huyo mtu, ule mwili (waliusulibisha huo, bali Mungu akaufufua), bali ilikuwa ni ule Uhai uliokuwamo ndani Yake. Yeye hakusema, “Njoni, mwone jinsi ninavyovalia nguo Zangu, hiyo ndiyo ishara Mimi ni Masihi. Njoni, mwone shule nilizotoka, kanuni ya imani ninayofundisha.” La, hivyo sivyo, vile alivyojitambulisha Mwenyewe. Bali Yeye alisema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Lakini ingawa ninazifanya kazi za Baba Yangu wala hamniamini, aminini zile kazi, ndizo zinazonishuhudia Mimi. Hizo ndizo zinazonitambulisha Mimi.” Nao waliona kwamba Wewe ulikuwa ni Masihi, kwa sababu Wewe ulikuwa ni Nabii, Mungu-Nabii.

<sup>184</sup> Na sasa usiku wa leo, Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utatubariki usiku wa leo kama ulivyombariki Kleopa na rafiki yake. Wakiisha kutembea pamoja na Wewe kwa muda wa miaka mitatu na nusu, na kuona mambo uliyofanya; halafu ulisulubiwa, chini ya Pontio Pilato—Pilato, ukateseka, ukasulubiwa, ukafa. Na siku ya tatu, walikuwa njiani kwenda Emau. Walikuwa wamesikia uvumi wa wanawake na baadhi ya wanafunzi, kwamba “Yeye alikuwa amefufuka.” Lakini siku hiyo ulitembea pamoja nao na kuzungumza nao waziwazi siku nzima. Hawakukutambua.

<sup>185</sup> Labda wengi hapa wamekuwa hivyo. Umetembea pamoja nao na kusema nao, wala hawakutambua Hilo.

<sup>186</sup> Lakini wakati jioni ilipowadia, wao walikualika ndani, ndipo ukaifunga milango na kuketi chini. Ndipo ukafanya jambo fulani vile vile tu ulivyolifanya kabla ya kusulubiwa Kwako. Wakajua basi ilikuwa ni Wewe. Dakika moja, ukatoweka machoni pao, ukaingia gizani. Hao wakawaendea watu wao, wakisema, “Bwana amefufuka!”

<sup>187</sup> Mungu, utafanya hivyo usiku wa leo tena? Fanya jambo fulani miongoni mwetu usiku wa leo, Bwana, kama tu ulivyolifanya kabla ya kusulubiwa Kwako. Ndipo tutakuwa na matumaini na kujua kwamba Kristo wetu hajafa, bali Yeye amefufuka kutoka kwa wafu, na yu hai hapa miongoni mwetu,

milele. Tunajikabidhi Kwako, Baba. Ninalikabidhi kanisa hili Kwako, na kila roho humu ndani, Kwako, upate kututumia kumheshimu Kristo. Katika Jina la Yesu naomba. Amina.

<sup>188</sup> Sasa kabla hatujaomba ama kuitisha mstari wa maombi, nitawaulizeni jambo fulani. Ninamtaka kila mtu, tafadhalini, kuendelea kuketi kwa dakika chache tu. Sasa hamna budi kuwa na uchaji mnamo wakati huu. Sasa, kama huamini, basi ponyoka uondoke polepole sana. Lakini sasa, kama utaamini, keti kimya, ninii tu ya ku-... yapata dakika kumi na tano, unaona. Hebu tuone kama Yeye atasema nasi. Sasa sisi, hatuko katika... Tuko katika uwanja wa maonyesho, bali hili ni kanisa. Limewekwa wakfu kwa kusudi hilo, kwa hiyo hebu tuketi kimya kabisa. Kila mmoja wenu ni roho. Kama sivyo, umekufa. Unaona? Kwa hiyo basi wewe ni roho, halafu basi wakati Roho Mtakatifu anaposhuka kutia mafuta miongoni mwa watu, Yeye huwasiliana, huwashika hao roho, mnaona. Nanyi mkisonga, kuna uhamisho.

<sup>189</sup> Mnasema, "Loo, Ndugu Branham!" Vema, kwa nini Yeye akamwongoza yule kipofu nje ya mji? Na, kwa hiyo, mnaona? Mnaona?

Sasa ni wangapi wanaomwamini? "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yeye."

<sup>190</sup> Sasa tunao mstari mdogo wa maombi tutakaoitisha. Ninaamini wanaita... Ni wapi... Ama alisambaza, naam, kadi za maombi moja hadi mia moja? Moja hadi mia moja, gani? C, C. Vema, hebu tuite baadhi yake, kadi za maombi. C, namba moja, ni nani aliye na kadi hiyo? C, namba moja. Angalia kadi yako ya maombi, wewe uliye na kadi ya maombi. Namba moja. Vema. Mtawaleta upande gani, hivi, nyuma hivi? Vema.

<sup>191</sup> C, namba moja. Namba mbili. Vema, mama. Namba tatu. Namba tatu. Kama unaweza kusimama, ama kuinua mkono wako ama kitu kingine, kusudi nita... Namba tatu, ni nani aliye na kadi ya maombi? Yule muungwana, vema. Namba nne, kadi ya maombi namba nne. Vema. Vema, namba nne. Ni nani aliye na namba nne, waweza kuinua mkono wako, tafadhali? Vema, mama, njoo hapa. Unaona, wananinii tu...

<sup>192</sup> Wao hushuka kuja huku, huyo mvulana huja, kisha anazichukua kadi hizi za maombi na kusimama mbele yenu. Anazichanganya pamoja, kisha anaanza tu kuwapa kadi ya maombi. Huenda ukapata sita, naye huyo mwingine apate kumi na nne.

<sup>193</sup> Njoo hapa, mama. Nne, tano. Halafu ni nani aliye na tano, inua mkono wako. Kadi ya maombi namba tano. Halafu jambo lingine wakati yeye... Papa hapa chini, ewe mama, hii. Halafu jambo jingine wanalofanya katika hilo, halafu wakati mwingine ninaita kutoka mahali pamoja... Ni wangapi wamewahi kuwa katika mkutano hapo awali, mmoja wa mikutano yetu? Loo,

vema, nilidhani nilikuwa miongoni mwa wageni. La hashu. Vema. Tano, sita. Ni nani aliye na sita? Vema. Saba, nane, nane, tisa. Ninapata hili, maana viziwi, na watu wako kwenye viti vya magurudumu wala hawawezi kutembea. Tisa, kumi, namba kumi. Kumi, tunasemaje hilo katika Kihispaniola? Kumi. Vema, kumi na moja, kadi ya maombi kumi na moja. Nilifikiri mtu fulani kwenye roshani. . . Hapa. Vema, kumi na mbili. Vema, kumi na mbili. Kumi na tatu. Kadi ya maombi kumi na tatu, unayo, mama? Kumi na nne, kumi na nne, kumi na tano. Hebu, vema, hilo, hebu tuanze namna hiyo sasa. Vema.

<sup>194</sup> Sasa, tafadhalini, iweni tu wenye uchaji sasa. Sasa ni wangapi humu ndani wasio na kadi ya maombi, na hata hivyo unaamini kwamba Yesu Kristo atakuponya? Inua mkono wako. Sijali mahali ulipo. Ni wangapi wamekuwa mikutanoni hapo awali, na wanajua kwamba wapo wengi wanaoponywa huko nje kuliko walio hapa juu, kwa kuwaita tu? Hakika, bila kadi za maombi! Iweni tu na imani sasa, msitie shaka, amini kwa moyo wako wote.

<sup>195</sup> Kadi ya maombi tano haipo. Bawabu anaita kadi ya maombi namba tano. Mnaona, kama ukiamka na. . . Usichukue kadi ya maombi isipokuwa utaitumia; unaona, usichukue. Chukua namba yako sasa, maana tutamwomba kila mtu aliye na hizo kadi, mnaona, na sisi—sisi hatutaki uikose fursa yako. Maana, sasa, tutakapoita tena sasa, tuliachia kwenye kumi na tano, hapo ndipo tutakapoanzia labda kesho usiku, mahali pale pale, mnaona. Tutazipata, kila moja, kwa hiyo basi uta—utaikosa fursa yako. Unaona? Naam. Kadi ya maombi namba tano. Vema.

<sup>196</sup> Basi kuwa tu na imani. Usitie shaka. Na uamini kwa moyo wako wote. Sasa, sasa kila mmoja wenu sasa aliye na kadi ya maombi, ama asiye na kadi ya maombi, nawe unaamini, sasa wakati wakiuandaa mstari, angalieni huku sasa.

<sup>197</sup> Wakati mmoja kulikuwako na mwanamke, na labda hakuwa na kadi ya maombi, bali alikuwa na kilichohitajika, imani. Basi akapitia kwenye umati, na akasema, “Kama ninaweza kugusa tu vazi Lake, nitapata afya.” Ni wangapi waliopata kuiskia hadithi hiyo? Yule mwanamke aliyetokwa na damu. Sasa maskini mwanamke huyo alikuwa ameyakinia atamgusa Yesu. Akasema, “Ninamwamini. Sijali ni wangapi wa makuhani na hao wengine wote hawamwamini, mimi ninamwamini. Na ninaamini kama ninaweza kugusa vazi Lake, nitapata afya. Ninaamini Yeye ndiye Masihi.”

<sup>198</sup> Mnaamini Yeye ndiye Masihi? Hakika. Sasa wewe unaweza kumgusa? Sasa, kwa wahudumu, wako wapi ndugu wahudumu? Vema, mhudumu, sasa ninii. . . Hivi Biblia inasema, ndugu wahudumu, ama ninyi nyote wasomaji wa Biblia, kwamba “Yeye sasa hivi,” Kitabu cha Waebrania, mlango wa 3, “ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu”? Ni

wangapi wanajua Biblia inasema hivyo? Hakika. Vema, basi, kama Yeye ndiye Kuhani Mkuu, na Kuhani Mkuu yule yule, hivi asingetenda vile vile? Mnaona? Kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, (hilo ndilo somo letu), Yeye angetenda vile vile. Sasa mnasema . . .

<sup>199</sup> Sasa kama ukija hapa juu na kunigusa, isingeleta tofauti hata kidogo. Ukiwagusa wachungaji, isingeleta tofauti hata kidogo. Ukingusa mchungaji wenu pale, yeyote yule, isingeleta tofauti hata kidogo. Lakini, mguse Yeye!

<sup>200</sup> Basi ungejua je ulimghusa? Yeye angerejea na kutenda kazi moja kwa moja na kufanya jambo lile lile. Unaona? Hebu mguse uone kama Yeye hatakujibu kupitia papa hapa, na kusema, “Imani yako; ulikuwa na *fulani-fulani*,” na chochote kilicho, na kukwambia kile kilichokuwa, na kile kilichotukia, na yote kuhusu hicho. Sasa, ni wangapi wameliona hilo likifanywa mara mamia, inua tu mkono wako. Mnaona? Hakika, kamwe halishindwi, kamwe halishindwi. Kwa nini? Yeye hawezi kushindwa; Yeye ni Mungu. Mnaona? Hivi huna furaha kuwa Mkristo, Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili, kweli pamoja na ushindi wa Kristo?

<sup>201</sup> Sasa, ninyi tu mlio huko kwenye kusanyiko sasa, iweni tu na kicho kabisa, na kusema, “Nitaliamini, haidhuru mtu mwingine yeyote anafanya nini, yale mtu mwingine yeyote asemayo, nitaliamini kwa moyo wangu wote.” Basi iweni tu waaminifu na kuamini sasa. Vema. Vema.

<sup>202</sup> Pale, wale ndugu pale nyuma, na wahudumu na hao wengine, wanawaleta wagonjwa.

<sup>203</sup> Sasa nafikiri, naam, *hii* ni hai. Sasa kama yule aliye kwenye . . . mhandisi kwenye hiyo ataiweka hiyo juu kidogo.

<sup>204</sup> Maana, wakati mwingine upako unaposhuka, basi si—sijui yale ninayosema. Mnaona, itanibidi ku . . . Ni mahali pengine huko nyuma maishani; mnaona. Halafu basi wakati mimi . . . Kama tu vile ulivyoiota, unaona. Nawe unaota kama ndoto, kama nikilifanya hivyo kwenu, hata hivyo umesimama papa hapa; na kurudi nyuma miaka kadhaa, katika maisha ya watu, na kuona waliyofanya, kuna tatizo gani, na chochote zaidi, na kulileta namna hiyo, mnaona. Na huyo ni Roho Mtakatifu. Ndipo Yeye anasema yale yaliyokuwapo, yaliyopo, yatakayokuwapo, kadhalika. Liangalieni tu na msikilize kwa makini, na mchukue kanda zenu, na Yeye atawaambia.

<sup>205</sup> Sasa huyu hapa mtu ambaye labda kidogo ana umri mkubwa kuliko mimi. Nami ninaamini hatufahamiani, mmoja kwa mwingine. Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana, ni juavyo mimi, mimi na wewe, hatufahamiani. [Huyo ndugu anasema, “Nimekuwa katika mikutano yako.”—Mh.] Umekuwa mikutanoni. Naam. [“Lakini sijawahi kukutana na wewe.”] Yeye amekuwa katika mikutano yangu, alisema, bali

hajawahi kukutana nami. Hakika, kuna mamilioni wamekuwa mikutanoni ambao kamwe nisingewajua. Lakini sisi, sasa hawa hapa wanaume wawili wanaokutana kwa mara yetu ya kwanza maishani. Yeye ni mwanamume tu anayesimama hapa, simjui. Hii hapa Biblia; si—simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye ameniona, kutoka mahali fulani kwenye wasikilizaji, mkutanoni mahali fulani. Lakini huyo hapo amesimama.

<sup>206</sup> Labda mtu huyu ni anayejifanya mwaminio. Labda yeye ni mwaminio. Labda yeye si mwaminio hata kidogo, hakuna njia. Labda yeye ni mwanamume tu. Labda ni mgonjwa, labda si mgonjwa. Labda ni tatizo la kinyumbani, tatizo la kifedha. Labda amesimama hapo kwa ajili ya mtu mwingine. Sijui. Lakini huyo hapo amesimama, nami huyu hapa.

“Sasa, mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.”

<sup>207</sup> Sasa, ningeweza kumfanyia nini mtu huyo? Sasa, huenda nikamwendea, nikaweka mikono yangu juu yake, nikasema, “Hivi wewe ni mgonjwa, bwana?” Angesema, “Naam, bwana.” Niweke mikono yangu juu yake, niseme, “Utukufu kwa Mungu, haleluya! Nenda, utapona. Haleluya!” Vema, sasa, hiyo inawezekana angepona; inategemea yale aliyowaza juu yake. Haidhuru, huenda ikawa... Mimi nikimtikisa na kuweka mikono yangu juu yake, haingefaa kitu. Ni imani yake katika Mungu ingefanya hilo. Lakini, sasa, yeye angekuwa na haki ya kutilia hilo shaka.

<sup>208</sup> Bali kama Roho Mtakatifu angesimama hapa na kumwambia jambo fulani ambalo limekuwa, kama vile Musa alivyoandika Mwanzo, basi hakika Yeye angeweza kumwambia yale yangekuwa. Angeamini hilo, sivyo? Sasa, sasa kama Yeye angefanya jambo hilo, kama Kristo angefanya hilo, ni wangapi wenu wangeamini kwa moyo wenu wote?

<sup>209</sup> Mnaona, sasa mnaona, kosa moja tu ninalopata Marekani, wameona mengi sana mpaka wanakuwa tu ni watazamaji, mnaona. Msifanye hivyo. Ninyi mheshimuni Kristo, mnaona. Msiniangalie mimi. Mimi ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Lakini sasa haidhuru Mungu angenitia mafuta jinsi gani, Yeye hana budi kumtia mafuta, pia. Hiyo ni kweli, haingefaa hata kidogo. Hana budi kumtia mafuta, pia. Hana budi kukutia mafuta, unaona, kukutia mafuta huko nje, Roho Mtakatifu akushukie.

<sup>210</sup> Halafu, huu ni mfereji tu. Wewe hulineni mwenyewe. Yeye ananena kupitia wewe. Ni mkondo ambao Mungu hutumia kunenea, mnaona. Ni kama maikrofoni hii, hiyo maikrofoni ni bubu isipokuwa kitu fulani hapa nyuma kinazungumza kuipitia. Basi, hiyo ni mimi, ninamjua mtu huyo? Sijawahi kumwona, lakini mimi ni bubu kwake. Mnaona?

<sup>211</sup> Kwa hiyo, “Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Sasa Yeye angefanya nini? Vipi kama mtu huyo ni mgonjwa, hivi Yeye angesema, “Nitakuponya”? Asingeweza kufanya hivyo; tayari amelitenda. Mnaona? “Kwa mapigo Yake sisi tuliponywa.” Alifanya hivyo pale Kalvari. Lakini angefanya jambo fulani kuonyesha ya kwamba Yeye angali ni Masihi. Hiyo ilikuwa ni kweli? Vema, basi, Yeye angefanya nini, hivi angesema, “Angalia makovu Yangu ya misumari”? Hivyo sivyo alivyosema hapo mwanzo. Yeye kamwe... Yeye aliwaambia tu yale yaliyokuwa moyoni mwao, na kadhalika, nao wakajua huyo alikuwa ni Masihi. Sasa huyo ni Yeye, yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>212</sup> Mnasema, “Ndugu Branham, kwani unangojea nini?” Yule Malaika wa Bwana. Hakika. Siwezi kufanya lolote. Ninamgojea. Asiponitia mafuta, siwezi—siwezi kusema lolote. Inategemea tu yale...

<sup>213</sup> Sasa Yeye yupo hapa. Yupo hapa sasa. Basi katika Jina la Yesu Kristo ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

<sup>214</sup> Sikujui wewe, bwana. Hatufahamiani. Lakini upo kitu fulani... ama unahisi kwamba jambo fulani linaendelea. Sasa mtu huyu asingeweza kuyaficha maisha yake. Yeye ni mgonjwa. Kumponya, siwezi mimi. Hakuna njia kwangu mimi kumponya. Huyu mtu amekuwa kwa da—daktari. Amefanyiwa uchunguzi. Hakika, anangojea upasuaji. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, bwana, inua mkono wako.

Mnaamini?

Unasema, “Ulibahatisha hilo, Ndugu Branham.” Sikubahatisha.

<sup>215</sup> Angalieni tena. Angalia upande huu, bwana. Ni kama tu Bwana wetu akizungumza na mwanamke, ni Roho Wake. Mimi si Yeye. Mimi ni mwanadamu kama ninyi, bali ni Roho Wake. Chochote alichokwambia, kilikuwa sahihi, chochote kile. Naam, hii hapa tena. Naam, naam, yeye yuko tayari kwa upasuaji sasa hivi, na ni tatizo la kibofu na tezi dume. Hiyo ni ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Unaamini sasa ya kwamba uko Uweponi Mwake? Vema. Nenda, ukiamini, nawe utapata afya. Amina.

Unaamini? Sasa ni rahisi tu hivyo kumwona Kristo akitenda kazi.

<sup>216</sup> Sasa, mama, sisi ni wageni mmoja kwa mwenzake. Huyu hapa... Umekuwa mkutanoni. Ninaposema “mgeni,” hilo linamaanisha mimi sikujui, wewe hunijui. Na mimi... Umeniona kwenye mikutano, na mambo kama hayo. Lakini kujua, kusema, “Naam, Ndugu Branham, wewe huja nyumbani kwangu, ninakujua, sisi ni marafiki wa karibu,” sikujui

jinsi hiyo. Nawe umekuwa tu mkutanoni mahali fulani. Nisingekuwa na fununu yoyote, sina habari juu yako, ni kwamba tu wewe ni mwanamke tu ambaye amekuwa katika mmoja, amehudhuria mkutano fulani mahali fulani. Sasa, kulikuwako na mwanamume. Huyu hapa mwanamke.

217 Hii hapa picha ya Yohana Mtakatifu 4, mwanamume na mwanamke wanakutana kwa mara ya kwanza maishani, kukutana uso kwa uso, kama mwanamke... yule mwanamke Msamaria na Bwana wetu Yesu. Sasa huyu hapa mwanamke, simjui. Sijawahi kumwona. Yeye ni mgeni kabisa. Mungu Mbinguni anajua jambo hilo. Sijawahi kumwona. Lakini kama Roho Mtakatifu atamwambia sababu ya yeye kuwa hapa, mtu mwingine ama chochote kile, ya nyumbani, ya kifedha, ninii... ama maradhi ama chochote kilicho, basi itambidi kukubali kwamba kuna Nguvu za kimbinguni hapa kufanya hilo. Hiyo ni kweli?

218 Mnaona, sasa inategemea kile unachodhania kuwa Ndicho. Unaweza kusema “Beelizebuli” ama unaweza kusema “Kristo.” Wewe, kama ukisema “Beelizebuli,” utapata thawabu yake. Unaona? Ukisema “Kristo,” ni thawabu Yake. Huna budi kuamini.

219 Sasa ni mahali pa jinsi gani linapokuweka! Kuna mtu anayetaka kupachukua mahali hapa? Kama huliamini, njoo hapa upachukue mahali pangu mara moja. [Ndugu Branham anatulia—Mh.] Sikuzote ni kusanyiko nyamavu hilo linapoulizwa.

220 Sasa, dada, angalia upande huu. Ni kwa nini nilikuika “dada” nilipoangalia huku? Nilikuwa nimekupa kisogo. Lakini nilimhisi Roho juu yako, kwamba wewe ni Mkristo. Wewe ni mwaminio. Sikujui mimi, bali ninajua wewe ni Mkristo. Kwa sababu, Roho aliye juu yako, na Roho aliye juu yangu, ni jamii moja, unaona. Wewe, unajisikia tu kama umekaribishwa, wajua, kumfanya tu ajisikie vizuri, umekaribishwa.

221 Sasa, iwapo Roho Mtakatifu, kama Yesu akizungumza na yule mwanamke kisimani, sisi hapa, mandhari ndogo tu kama kile kisima huko Sikari, nilichokuwa nikinena habari zake. Sasa, kwa kuwa sisi sote ni waaminio, nasi tumesimama hapa, Roho Mtakatifu akiwa juu yetu sote wawili. Sasa Yeye ametoa... Mimi si mhubiri. Ila Yeye hunipa karama; hayo ndiyo mahubiri yangu. Ni karama ya kinabii. Na hizi ni za muda tu; itahitaji imani yako kufanya hivyo; kama yule mwanamke aliyeligusa vazi Lake, kasema, “Imani yako imekuokoa,” unaona. Sasa, hilo ndilo jambo lile lile linalohitajika sasa, unaona, inahitaji imani yako. Ndipo Yeye ananiambia jambo fulani, mahali pa kwenda na mahali mbalimbali.

222 Sasa, hapa, Yeye alikuwa na haja kupitia Samaria. Sasa niko njiani kwenda Alaska, bali nilikuwa na haja kuja huku. Kwa

nini? Nilijisikia kuongozwa kuja hapa. Nami huyu hapa; wewe hapa umekuja jukwaani. Hivyo ndivyo tu nijuavyo. Nawe huyu hapa umesimama. Wewe ni Mkristo nami ni Mkristo, sote wawili tukiwa na Roho Mtakatifu. Nalo hili hapa Neno Lake, kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

<sup>223</sup> Sasa, kama Yeye atakufunulia jambo fulani lililo maishani mwako, utajua kama ni kweli ama si kweli. Naye atakufanya kuamini basi kwa ajili ya chochote unachoombea; maana Mkristo asingesimama hapo namna hiyo, una—una haja ya kitu fulani la sivyo usingesimama hapo.

<sup>224</sup> Kila mtu mwingine ataamini? Kuna mtu anayemfahamu mtu huyu? Naam, watu wengi wanamfahamu huyu mtu.

<sup>225</sup> Vema, kulingana na madaktari, unapaswa kufanyiwa upasuaji, pia. Ni vivimbe. Hiyo ni kweli. Unaamini Roho Mtakatifu anaweza kunifunulia mimi mahali vivimbe hivyo vilipo? Mafigo. Hiyo ni kweli. Sasa unaamini? Wewe hutoki hapa. Umekuja hapa yapata maili mia mbili ama mia tatu. Ulifanya safari ndefu kufika hapa. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Isitoshe, jambo lingine, wewe ni mke wa mhudumu. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? Ingekusaidia? Bibi Johnson. Nenda, ukiamini, ukaponywe; na kwa moyo wako wote.

<sup>226</sup> Unaamini kwa moyo wako wote? Unaona? Yesu Kristo! Mabwana, sisi tunataka kuona... Mnasema, “Vipi hivyo?” Vema, hayo si zaidi ya yale Yeye aliyowaambia hao wengine. Mnaamini? “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Huyu ni Yeye. Sasa nendeni mkazungumze na huyo mwanamke, mkamwulize.

<sup>227</sup> Sasa huyu hapa mwanamume, mgeni kabisa, simfahamu, kamwe sijawahi kumwona maishani mwangu. Huenda ameliwa na kansa, huenda akawa na matatizo ya kinyumbani, kifedha. Sijui ana shida gani. Amesimama hapa, mwanamume tu. Sasa iwapo Roho Mtakatifu atamfunulia mtu huyo, mwajua. . .

<sup>228</sup> Maskini mama yule anayeketi nyuma kabisa hapa kuelekea mahali ninapokielekeza kidole changu, anayeugua huo ukurutu. Laiti ungaliamini kwa moyo wako wote! Unaliamini, mama, kwa moyo wako wote? Maskini mwanamke mwenye mvi aliyevaa miwani, anao, anaugua ukurutu. Alikuwa amesimama pale, ama ameketi pale, hasa, akiwazia alikuwa na kasoro gani, akiomba moyoni mwake. Na sasa kama hiyo ni kweli, nawe unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, simama kwa miguu yako.

<sup>229</sup> Yeye aligusa nini? Ninawaulizeni, aligusa nini? Yuko yadi ishirini kutoka kwangu. Yeye alimgusa Kuhani Mkuu, naye huyo Kuhani Mkuu yupo hapa! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hivi hamwoni? Msilitilie shaka. Liaminini! Iweni na imani.

<sup>230</sup> Sasa, nisingeweza kusaia hilo, bwana. Ni kwamba tu ni—ninaiangalia Nuru, mnaona, na Hiyo iliondoka tu kwangu,

nami nikaiona ikining'inia kule, nami nikamwona maskini yule mama akiya hapa juu mbele yangu. Naye akaendelea kuja mbele zangu hapa, nami nikaona ilikuwa ni mwanamke badala ya mwanamume, kwa hiyo ilinibidi tu kusema yale niliyokuwa nikiona.

<sup>231</sup> Loo, laiti kanisa hili, laiti kundi hili la watu lingeamini tu sasa hivi, na liwe tu na imani, ni jambo gani lingalitukia, ingekuwa je!

<sup>232</sup> Bwana, sisi hatufahamiani. Nilitaka tu kuzungumza na wewe, kusudi tu niwasiliane na roho yako. Hapa, hupo hapa kwa ajili yako mwenyewe. Upo hapa kwa ajili ya mtu mwingine, huyo ni jamaa m—mdogo, jamaa mdogo, mvulana mdogo ambaye ameumia sana katika ajali ya motokaa, akakatakatwa vipandevipande, akajeruhiwa sana, hawezi kabisa, hali mahututi. Wewe upo hapa, ukisimama kwa niaba yake. Hiyo ni kweli. Mungu asipomsaidia mvulana huyo mdogo, hana budi kufa. Utanifadhili? Chukua lesa hiyo kutoka mfukoni mwangu; nenda, kaiweke juu yake, katika Jina la Bwana, na usitie shaka. Pia naomba nisikie kutoka kwake, wakati mkutano ukiendelea. Uwe na imani.

<sup>233</sup> U hali gani, bwana? Hatufahamiani. Mwanamke mwingine. Hivi unaamini? Sasa, kumbukeni, Yeye ni yeye yule tu huko kadiri alivyo hapa. Yuko kotekote. Yuko kila mahali.

<sup>234</sup> Dada Borders, ndiwe unayeketi hapo? Sioni vizuri. Ilionekana kana kwamba ni Dada Borders anayeketi pale. Siwezi... Roy, mke wa Ndugu Roy Borders. Nadhani siye. Ilienda moja kwa moja, ikasimama juu ya yule mama. Sasa, hebu kidogo tu, na labda itaita tena, tuone itakalofanya.

<sup>235</sup> Sikufahamu. Bwana anatumia sote wawili. Kama Bwana atanielezea, na kufanya jambo fulani hapa, ambalo ndilo lililokuleta hapa, hivi utaamini kwa moyo wako wote? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.]

<sup>236</sup> Bibi Borders anaendelea kusimama hapa mbele zangu, mahali fulani. Mimi... Bibi Borders yuko mkutanoni mahali fulani. (Mke wako ana tatizo lolote?) Vema, linaendelea tu kuja hapa. Pia kuna kundi la watu, mtu fulani karibu naye, nami naendelea kushangaa.

<sup>237</sup> Unaugua kivimbe. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kivimbe hicho kiko wapi? Kwenye nyonga. Amini kwa moyo wako wote. Una matatizo ya ziada, pia, mambo mengine mengi. Wewe amini. Hiyo ni kweli. Unaamini kwa moyo wako wote? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Nenda, ukiamini namna hiyo, nawe utaninii... utakwisha, na Mungu atakuponya na kukupa afya. [Dada huyo anasema, "Ndugu Branham, yule mwanamke alikuja pamoja nami, mwenye ukurutu, alikuja pamoja nami. Nami sikujua mpaka tulipoketi pale nyuma, akasema alikuwa na ukurutu."] Mnaona,

kuchangamshwa kwake kwa kuingia katika mstari wa maombi labda ndiko kulikosababisha hilo, kuombeana.

238 Hili hapa! Loo, ninaona! Nimemwona Bibi Borders amesimama hapa. Yeye anaomba. Na kuna mmoja—mwanamke mmoja anayeketi karibu naye, ambaye anaomba, yeye ana shinikizo la chini la damu. Iwapo unaamini, unayeketi papo hapo, mama, kwa moyo wako wote wewe liamini, na Mungu atakupata afya, uliye na shinikizo la chini la damu. Amina. Haya basi. Hapo ndipo hayo maombi yalipokuwa yakitoka.

239 Kama utaniamini mimi kuwa ni nabii, ama, samahani, mtumishi, (hilo huwakwaza watu), weka mkono wako juu ya huyo mwanamke anayeketi karibu nawe, kwa sababu anaugua ugonjwa wa mishipa ya damu. Mnaona, hiyo ni kweli. Amina.

240 Amini kwa moyo wako wote sasa! Niambieni kile wanachogusa; maskini mwanamke anayeketi pale, wakiombeana, inaendelea kujitokeza jukwaani. Amini tu kwa moyo wako wote! Vema.

241 Njoo hapa, mama. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini? Unaamini ya kwamba ugonjwa huo wa tumbo utapona? [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Basi nenda ukale chakula chako cha jioni. Yesu Kristo anakuponya.

242 Unaamini nini? Unaamini kwamba Mungu atauponya ugonjwa huo wa mgongo, hayo mafigo, na kukupa afya? Nenda nyumbani, ukiamini, useme, “Yesu Kristo ananiponya.” Uwe tu na imani, usitie shaka.

243 Njoo, bwana. Ulikuwa na furaha sana ulipotoka kwenye ule mstari pale, wakati namba yako ilipoitwa. Mungu huponya ugonjwa wa moyo na anaweza kukupa afya. Unaamini hilo? Basi nenda zako, ukiamini, na yote yatakuacha, nawe uta—utapata afya. Vema.

244 Kuwa na imani. Usitie shaka, Mama, unawazia nini kulihusu? Unafikiri kama nikiweka mikono yangu juu yako, utapata afya? Kama tu sikusema lolote, niweke tu mikono yangu juu yako? [Dada huyo anasema, “Hata si lazima uniwekee mikono.”—Mh.] Endelea. “Sio lazima,” vema, hilo ni jema. Nenda moja kwa moja. Amina. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Vema.

245 Njoo, mama. Unaamini nini, dada? Unaamini kwa moyo wako wote? Unajua Mungu anaweza kuniambia una shida gani, lakini utaamini? Basi kisukari si kitu kwa Mungu, Yeye anaweza kukiponya. Unaamini hilo? Vema, endelea, ukapone. Amina.

246 Vema, bwana. Njoo, bwana. Hatufahamiani. Kila mtu hukwambia, “Jirudie,” kwa kuwa wewe una wasiwasi. Lakini huwezi kujirudia, kuna kitu fulani mle kinachokutia wasiwasi. Hiyo ni kweli. Lakini unasimama mahali sasa ambapo

umekuacha sasa. Nenda, ukiamini, nao hautarudi tena. Nenda, amini hilo. Amina. Kuwa na imani. Usitie shaka. Vema.

<sup>247</sup> Mambo mengi, tatizo la wanawake, baridi yabisi. Sasa unaamini Mungu atakupa afya? [Huyo dada anasema, “Amina.”—Mh.] Nenda tu, ukisema, “Mungu asifiwe,” na—na uamini kwa moyo wako wote.

Njoo, mama.

<sup>248</sup> Ninyi mnaamini huko nje? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Mungu anaweza kuponya kisukari, chochote katika damu. Hivi huamini hilo? Hakika, Yeye anaweza. Endelea moja kwa moja, ukiamini, ukisema, “Amina! Bwana asifiwe!”

<sup>249</sup> Unaamini, “Weka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya”? Katika Jina la Bwana Yesu, nenda, ukapone sasa, na uamini kwa moyo wako wote.

<sup>250</sup> Vema, njoo moja kwa moja, bwana. Unaamini Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo; afanye tezi dume, kila kitu, huo wasiwasi na kila kitu kikuache? Basi nenda, liamini katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

<sup>251</sup> Unaamini kwa moyo wako wote? Nanyi wengine je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.]

<sup>252</sup> Viwete wenu wako wapi? Ninaona kiti cha magurudumu. Wasemaje, bwana? Niangalie mimi hapa. Unaniamini? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Unaamini. Niangalie, basi. Ni, tatizo lako ni miguu yako. Unapaswa kwenda, hospitalini; bali usingeenda, kwa sababu ulifikiri kama ungeweza kufika hapa, ungepona, wala haingekubidi kwenda hospitalini. Hiyo ni kweli. Unaliamini? Kama ukiketi hapo, una hakika ya kufa; kama wale wenye ukoma. Daktari hawezi kukusaidia hata kidogo. Kwa hiyo kwa nini usimkubali Kristo usiku wa leo, na uamini kwa moyo wako wote, kisha usimame toke kwenye hicho kiti cha magurudumu, na ushike mwisho wake na kukisukuma huku, na utoke mlangoni uende nyumbani, ukawe mzima? Mbona usifanye hivyo? Utaliamini? Basi simama. Usitie shaka. Katika Jina la Yesu Kristo, chukua kiti chako cha magurudumu uende nyumbani!

<sup>253</sup> Unaamini kwa moyo wako wote? Simama kwa miguu yako, mtu yeyote anayetaka kuponywa. Simameni kwa miguu yenu, na mliamini. Simama! Sijali una shida gani, jinsi ulivyolemaa. Hilo halileti tofauti yoyote. Ninawapa changamoto, simameni! Simameni, kila mtu, kila kiwete, popote ulipo. Katika Jina la Yesu Kristo, simameni kwa miguu yenu mpate kuponywa! Haya basi, kusanyiko lote, limesimama.

<sup>254</sup> Sasa hebu tumwinulie Mungu mikono yetu. Baba wa Mbinguni, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu. Wewe huyu hapa! Hakuna mtu mnyonge miongoni mwetu, kila mtu

ameponywa. Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Baba! Sasa tunaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utamshinda ibilisi kwa kila hali sasa, uondolee mbali kutokuamini kwote.

<sup>255</sup> Shetani, katika Jina la Yesu, liache kusanyiko hili, toka mahali hapa! Umeshindwa vita. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, jalia waponywe, kila mmoja wao. 

62-0704 Sisi Tunataka Kumwona Yesu  
Municipal Auditorium  
Grass Valley, California Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)